Nipashe

Jumatatu Februari 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581598

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


Nipashe
Spotika
ALONSO UKURASA 12-13
NYOTA WA5 WATAKAOTIKISA USAJILI MAJIRA YA JOTO 2024

UKURASA 11


**Idadi** ya watalii wanaoingia Zanzibar yazidi kupaa



UKURASA 17

**NMB** yang'ara Tuzo za Mwaka Ubora Huduma

UKURASA 8



**Serikali** yaonya watoto kubebeshwa 'zigo' begi la madaftari

UKURASA 15

# HATIMAYE

• **UMEME** Bwawa la Nyerere rasmi Gridi ya Taifa, Biteko 'meno nje' mtambo ukiwashwa... *Endelea Ukurasa 2*



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, akiangalia maji yaliyojaa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere jana. Kushoto kwake ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bibi harusi afa ajali ya Arusha, vifo vyafika 25

UKURASA 3



Fathiya Chucha (23) aliyekuwa bibi harusi, akiwa ni mmoja wa waliopoteza maisha katika ajali iliyotokea Arusha mwishoni mwa wiki.

## Bei ya sukari kubandikwa barabarani



UKURASA 4

**MICHEZO** **GAMONDI APANIA KUIDUWAZA AL AHLY** UK.24

**MAONI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Rais wa Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier, wakati wa mazishi ya aliyekuwa Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingob, katika Uwanja wa Michezo wa Uhuru jijini Windhoek mwishoni mwa wiki. **PICHA: IKULU**

# Umeme Bwawa la Nyerere waingizwa Gridi ya Taifa

**Na Salome Kitomari**

HATIMAYE serikali imeingiza megawatt 235 kwenye Gridi ya Taifa ambazo zimepunguza mgawo wa umeme kwa asilimia 85, baada ya kuwasha mtambo namba tisa kati ya idadi hiyo inayowezeshwa jumla ya megawatt 2,115.

Vilevile, imeelezwa kuwa Machi mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Misri, Abdel-Fatah Alsisi, watazindua mtambo namba nane na hivyo kuwezesha nchi kuwa na megawatt za nyongeza kwenye Gridi ya Taifa kuwa 470.

Akitangaza hatua hiyo jana mbele ya wahariri wa vyombo vya habari, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, alisema kwa sasa upatikanaji umeme nchini ni wa asilimia 98, mgawo umepungua na utakwisha siku za karibuni.

"Leo (jana0 nchi inaingia kwenye historia, mradi ulioanza kujengwa tangu mwaka 2015 unaanza kutoa umeme.

"Ninamshukuru Mungu kwa hatua kubwa, ninamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alikuta mradi ukiwa asilimia 33 ya utekelezaji na kuhakikisha fedha zinapatikana na mkandarasi kulipwa kwa wakati.

"Ninafurahi kusema kile nilichokuwa nimeahidi kwamba Februari 25, mtambo namba tisa unaingiza megawati 235 kimetimia. Hii ni kutokana na msukumo mkubwa.

"Kwa ratiba tuliyokuwa nayo ya kawaida, umeme huu ungetufikia mwezi wa sita (Juni) ila kwa msukumo mkubwa wa Rais Samia leo (jana) tumefanikisha," alisema.

Waziri Biteko alisema upungufu uliokuwapo ni megawatt 200 hadi 400, hivyo kutakuwa na umeme wa ziada megawatt 70, na kwamba kuanzia mwezi wa tatu hakutakuwa na mgawo kabisa nchini.

"Kwa hatua ya kuingia huu mtambo, upungufu wa umeme umeshuka kwa asilimia 80, ninafurahi kuwaambia watanzania uwekezaji umejibu, tumepata umeme pamoja na siasa nyingi na magumu tuliyopitia.

"Ninawapongeza sana TANESCO (Shirika la Umeme) na TANROADS (Wakala wa Barabara nchini) na makandarasi. Tungefuata taratibu na ratiba ya kawaida tusingekuwa hapa. Wamefanya kazi kuhakikisha mradi unafikia hapa.

Tutasimamia vyanzo vya maji kuhakikisha maji yanapatikana wakati wote.

"Jambo muhimu watanzania wanataka umeme, hawataki maneno, tumechagua kutenda zaidi kuliko kusema," Dk. Biteko alisema.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, mahitaji ya umeme yanaongezeka na serikali imeongeza vyanzo vingine vingi kwa lengo la kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana.

"Nchi iko kwenye mikono salama na changamoto zitaendelea kutatuliwa," alisema Biteko na kusisitiza kuwa ndoto ya serikali ni kujenga uchumi wa viwanda kwa sababu vijana wanaomaliza, hawawezi kupata ajira kama hakujengwi viwanda nchini.

Alifafanua kuwa ili kufanikisha hilo, ni lazima kuwe na nishati ya uhakika, na ili iwe ya uhakika ni lazima kuwa na vyanzo vingi vya nishati.

"Mkuu wa Mkoa wa Pwani amesema kuna ongezeko la viwanda vipya 30 kwa kipindi cha serikali ya awamu ya tano na sita huku viwanda 17 viko katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji, maana yake utajitajika umeme mwingi zaidi.

"Tunawapongeza viongozi wetu Hayati John Magufuli na Rais Samia kwa kusukuma mradi huu ukamilike.

"Niwaombe sekta zote tufanye kazi kama serikali moja, wananchi wanahitaji majibu, tuwape huduma bora ili kuwaondoa kwenye umaskini," aliagiza Dk. Biteko.

Meneja wa Mradi wa Pamoja Baina ya Tanzania na Kampuni za Elsewedy Electric na The Arab Contractors, Mohamed Zakya, alimpongeza Naibu Waziri Mkuu Biteko kwa kusukuma kuhakikisha mtambo namba tisa unawashwa.

"Mheshimiwa, juhudi zako nimeziona, umetusukuma hadi tumefanikiwa, hatukutarajia kwamba itawezekana ila leo (jana) tuna furaha kubwa kwamba tumefanikisha ulichoagiza na kuhakikisha matakwa ya nchi yanatimia," alisema.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema jukumu kubwa ni kuhakikisha maji yanapatikana na kunapokuwa na matatizo ya umeme sekta nyingine zinatikisika.

Kwa hali ilivyokuwa, walitikisika.

Alisema Bwawa la Nyerere linahitaji lita za ujazo bilioni 32.7 na kwamba hadi sasa maji maji yaliyoingia ni lita za ujenzo bilioni 28. Kupitia Bonde la Mto Rufiji, maji yatafika kiwango kinachotakiwa.

"Tukiwa na maji toshelevu, tuna uhakika wa nishati. Ni jukumu letu sote kulinda na kutunza rasilimali maji, fedha zilizowekezwa hapa ni nyingi sana.

"Tumeshuhudia Dar es Salaam Mto Ruvu ulikauka, mabadiliko ya nchi yapo. Utunzaji unaanza na mimi na wewe na sisi sote. Kwa haya ninayoyaona, Dk. Suluhu ni suluhu ya watanzania," alisema.

Alizitaka mamlaka za maji kutoa taarifa kwa wananchi kunapokuwa na changamoto za maji.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema kuna viwanda 1,533. Kati yake, vikubwa ni 120, vya kati 124 na vingine vilivyobakia ni vidogo, hivyo mahitaji ya umeme ni makubwa na kuna wakati wamiliki walitishia kufunga viwanda kutokana na changamoto ya umeme.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) una thamani ya Sh. trilioni 6.6. Unatarajiwa kumaliza tatizo la muda mrefu la mgawo wa umeme nchini, pia kuuza umeme kwa nchi jirani, ukizalisha MW 2,115.

**KUPOTEA KWA CHETI**



**EDWARD BONIPHACE NGOWI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHA SHULE YA SEKONDARI BISMARCK ILIYOPO WILAYA YA **NYAMAGANA** MKOANI MWANZA CHENYE NAMBA **S.1194/0044/2016** KILICHOTOLEWA NA NECTA.
YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA RB NAMBA **PHQ/MWA/NYA/4051/2024.**

# Ziara ya Waziri Mkuu kutikisa watendaji Mara kwa siku tano

**Na Vitus Audax**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa leo anaanza ziara ya kikazi ya siku tano mkoani Mara, akitembelea na kukagua miradi ya maendeleo katika halmashauri zote za mkoa huo.

Katika ziara hiyo, Waziri Mkuu anatarajiwa kukagua mradi wa maji mkubwa wa Sazira, maendeleo ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma na kutembelea nyumbani kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere, Mwitongo, wilayani Butiama.

Akitoa taarifa ya ziara hiyo jana, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda alisema Waziri Mkuu anatarajiwa kuzungumza na watumishi na viongozi mkoani Mara, kufanya mikutano ya hadhara, kutembelea, kukagua, kuweka mawe ya msingi na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za utawala, elimu, afya na miundombinu.

Mtanda alisema Waziri Mkuu atazungumza na wananchi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mara ikiwamo mkutano mkubwa wa hadhara utakaofanyika Uwanja wa Shule ya Sekondari Mara, mjini Musoma Februari 29.

Alisema kuwa leo Februari 26, Waziri Mkuu atasalimia wananchi eneo la Mariwanda kabla ya kutembelea na kukagua Shule ya Msingi Sabasita iliyoko katika eneo hilo, atakagua na kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mara, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Vilevile, Majaliwa atakagua na kuzindua mradi wa maji wa Sazira na kufanya kikao na watumishi na viongozi kisha kufanya mkutano wa hadhara katika uwanja wa Shule ya Msingi Miembeni, mjini Bunda.

Alisema ziara itaendelea Februari 27, Waziri Muu atakagua na kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama, kufanya kikao na watumishi na viongozi, kuwasalimia wananchi wa Butiama na kutembelea nyumbani kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere, huko Mwitongo, Butiama.

Pia atakuwa na kikao na watumishi pamoja na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti na kuzungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara utakaofanyika Uwanja wa Sokoine, Mugumu na baadaye kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Getarungu.

Mtanda alisema baada ya hapo, Waziri Mkuu ataelekea Nyamwaga ambapo ataweka jiwe la msingi katika jengo la utawala Halmashauri ya Wilaya ya Musoma na kusalimiana na wananchi kisha ziara itaendelea Feburuari 28 ambapo atatembelea na kukagua mradi wa maji Komuge na baadaye kutembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kabla ya kufanya mkutano wa hadhara katika eneo la Utegi.

Alisema Waziri Mkuu atafanya mkutano wa hadhara katika eneo la Sirari na kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa soko la kimkakati la Mji wa Tarime na kufanya mkutano wa hadhara katika Uwanja wa Serengeti katika Mji wa Tarime na Februari 29 atakagua ujenzi wa Uwanja wa Ndege Musoma kisha ataelekea Kijiji cha Suguti kuweka jiwe la msingi katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma.

"Hapo atazungumza na viongozi na watumishi kisha ataelekea Kijiji cha Bwai kwa ajili ya kuzungumza na wananchi na kuhitimisha ziara yake katika Manispaa ya Musoma ambapo atafanya mkutano wa hadhara katika Uwanja wa Shule ya Sekondari Mara," alisema Mtanda.

Ziara za Waziri Mkuu zimekuwa zikiambatana na hatua za kuchukuliwa hatua watendaji wa serikali wanaobainika kutumia vibaya madaraka, kufuja mali ya umma au kushindwa kusimamia utekelezaji wa miradi na mipango ya serikali.

HABARI KITAIFA

# Bibi harusi afa kwa ajali Arusha, vifo vyafikia 25

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

VIFO vilivyotokana na ajali ya barabarani katika Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha vimefikia 25, huku mmoja wa waliopoteza maisha akiwa ni bibi harusi mtarajiwa, Fathiya Chucha (23).

Vilevile, kati ya majeruhi waliolazwa katika Chumba cha Wagonjwa Wanaohitaji Uangalizi Maalum (ICU) cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Mount Meru), inaelezwa kuwa yumo bwana harusi, ambaye anapigania uhai wake.

Ajali hiyo iliyoacha simanzi na vilio katika Mkoa wa Arusha, ikisababisha ulemavu kwa baadhi ya majeruhi 21, ilitokea juzi saa 11:00 jioni katika eneo la Kibaoni Bypass, Ngaramtoni ya Juu, Barabara Kuu ya Namanga/Arusha.

Jana Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Awadhi Juma Haji, baada ya kufika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru) kutoa pole kwa majeruhi, alisema vifo 10 zaidi vimeongezeka kutoka 15 vilivyoripotiwa juzi baada ya kutokea ajali.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni lori la mizigo lenye namba za usajili KAC 943 H, aina ya Mack lililokuwa linavuta tela lenye namba za usajili ZF 6778, kuyagonga magari mengine yaliyokuwa mbele yake.

Lori hilo la masafa marefu, mali ya kampuni ya KAY Construction ya Nairobi, Kenya, liligonga basi dogo la abiria (daladala) aina ya Nissan Caravan, namba T 879 DBY kisha likagonga gari dogo, aina ya Mercedes Benz (saloon) na baadaye basi la wanafunzi la Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya New Vission, aina ya Toyota Coaster, namba T 673 DEW lililokuwa na raia wa kigeni pamoja na watanzania.

Kwa mujibu wa Kamishna Awadhi, uchunguzi wa awali unaonesha kuwa lori hilo lilifeli breki, kitendo ambacho kilisababisha kwenda kuyagonga magari mengine.

Alisema jeshi hilo linaendelea kumsaka dereva wa lori hilo lililosababisha ajali, ambaye alikimbilia kusikojulikana muda mfupi baada ya ajali.

Kamishna Awadhi aliwataja waliofariki katika ajali hiyo kuwa ni wanaume 14, wanawake 10 na mtoto mmoja wa kike, huku raia wa kigeni waliofariki dunia wakitambuliwa ni saba.

**RAIS SAMIA**

Juzi Rais Samia Suluhu Hassan katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii aliandika: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya vifo vya watu 15 katika ajali iliyohusisha magari manne eneo la Ngaramtoni, mkoani Arusha.

"Ninatuma salamu za pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa waliopoteza jamaa zao katika ajali hii. Ajali hizi zinachukua wapendwa wetu, nguvukazi ya taifa na mihimili ya familia.

"Ninaendelea kutoa wito kwa kila mmoja kuzingatia sheria za usalama barabarani katika matumizi ya vyombo vya moto.

"Ninaagiza vyombo vyetu vya ulinzi, usalama na udhibiti kuendelea kuhakikisha vinasimamia sheria kikamilifu, ikiwamo ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri na udhibiti wa leseni kwa madereva wanaorudia kuvunja kuvunja sheria mara nyingi, na wakati mwingine kusababisha watu kupoteza maisha."

**BIBI HARUSI**

Katika ajali hiyo, familiya ya Latipha Mphoy, mkazi wa Kijenge Mwanama, jijini Arusha, imempoteza mtoto wao, Fathiya Chucha, aliyetarajia kufanya sherehe ya kuagwa kabla ya harusi (send off) Aprili 18, mwaka huu.

Simulizi kuhusu utambuzi wa mmoja wa waliopoteza maisha katika ajali hiyo kuwa ni bibi harusi mtarajiwa, imetokana na kundi sogezi la waliosoma Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kibosho mwaka 1995 (Kibosho Girls), kupewa taarifa ya mwanachama mwenzao kufiwa na mwanawe waliyekuwa wakimchangia fedha za kuendesha shughuli ya 'send off'.

Katika taarifa hiyo iliyochapishwa saa 2:18 usiku wa Februari 24 na Mwenyekiti wa Kundi hilo la Kibosho Girls, Asha Zulu, kulieleza kuwa ajali hiyo imeondoa maisha ya bibi harusi mtarajiwa, Fathiya Chucha; mtoto wa mwanakikundi mwenzao Latipha Mphoy, aliyekuwa kwenye gari dogo aina ya Mercedes Benz.

Kwa mujibu wa andiko hilo la kiongozi wa kundi hilo, mwili wa Fathiya ulitarajiwa kuzikwa jana saa saba mchana huko Kijenge Mwanama, jijini Arusha.

**KONDAKTA ALONGA**

Kondakta wa lori la mizigo lililosababisha ajali hiyo, Jastas Juma, raia wa Kenya, akisimulia hali ilivyokuwa, alisema lori lao halikuwa bovu kama inavyodaiwa.

Shuhuda huyo aliiambia Nipashe jana kuwa wakiwa njiani maeneo ya Oldonyo Sambu, moja ya magurudumu lilipata pancha na kubadilishwa na kuendelea na safari hadi walipofika Arusha Bypass, wakashtukia gari halishiki breki.

"Nikaanza kupiga kelele watu wapishe maana gari halina breki nikashtukia nimetupwa mtaroni na sikufahamu kilichoendelea na kujikuta baada ya muda nipo wodini," alisema Jastas. Walikuwa wanatokea Kenya kuelekea Dar es Salaam.

"Baada ya ajali mimi sikujua dereva wangu alikwenda wapi. Mimi nilijikuta tu niko kwa hospitali," alisema Jastas.

Mashuhuda wengine ambao ni majeruhi wa ajali hiyo, raia wa Togo, Apelo Apeto na Paulo Dino, raia wa Nigeria, kwa nyakati tofauti walieleza kuwa walikuwa wakitoka Shule ya New Vission iliyoko Ngaramtoni na walikuwa huko kwa ziara ya mafunzo.

"Nikiwa eneo la tukio nilisikia kishindo cha gari na sikufahamu kilichoendelea, lakini ninawashukuru madaktari na wauguzi kwani nimepata huduma nzuri na sasa ninaweza kuongea," alisema Apeto. Alisema ziara yao ilishafikia mwisho na ilikuwa ifikapo Ijumaa wiki hii wangerejea kwenye mataifa yao.

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Juma Sagini, alimwagiza Kamishna wa Polisi wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Awadhi, kuhakikisha magari yote ya mizigo yanakaguliwa kwenye mipaka ya nchi inapofika ili kuepusha ajali zisizo za lazima.

Aliagiza askari wa usalama barabarani wasisubiri wiki ya usalama barabarani kufanya ukaguzi, bali iwe desturi ya kila mara kwa magari ya ndani ya nchi.

"Lori hili lingekaguliwa Namanga pale mpakani lisingekuja kutusababishia ajali hapa kwetu limetoka huko likiwa bovu, hata kwa kuliangalia ni chakavu, lingekaguliwa haya yasingetokea, sasa ukaguzi ufanyike mipakani kwa magari haya ya mizigo," aliagiza.

***Imeandaliwa na Cynthia Mwilolozi, Godfrey Mushi (ARUSHA) na Idda Mushi (MOROGORO).**


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA TAFSIRI KATIKA KAMPUNI YA EACOP LTD NCHINI TANZANIA - KUMBUKUMBU NA. 00000481

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD, kampuni ya mafuta na Gesi, inakaribisha kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma za Tafsiri katika Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EAOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalosafirisha mafuta ghafi Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, karibu na Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, ambapo kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania bomba litapita katika mikoa minane (8) inyojumuisha mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**

- Mtoa huduma lazima awe na ujuzi wa lugha na uwezo wa kutafsiri nyaraka kwa ufasaha katika lugha za, lakini sio tu, Kiingereza, Kiswahili, Kifaransa na Kichina.
- Kuonyesha ujuzi katika istilahi za kiufundi na za tasnia mahususi zinazohusiana na sekta ya mafuta na gesi.
- Kutafsiri aina mbalimbali za nyaraka, ikiwa ni pamoja na nyaraka za kisheria, kiufundi, kimazingira na nyaraka zinginezo zinazohusu masuala mbalimbali.
- Kutekeleza mchakato thabiti wa uhakiki wa ubora ili kuhakikisha tafsiri sahihi na faafu zenye kuendana na utamaduni.
- Kutoa huduma za kusoma na kuhariri ili kudumisha viwango vya ubora wa juu.
- Kuzingatia muda uliowekwa kwa ajili ya ukamilishaji wa nyaraka zilizotafsiriwa.
- Kuwasiliana mara moja endapo kutatokea ucheleweshaji usiotarajiwa na kupendekeza muda mbadala.
- Kutunza siri za nyaraka na taarifa zote zinazopokelewa wakati wa mchakato wa kutafsiri
- Kutayarisha njia za mawasiliano zilizo sahihi na zinazofaa kwa jili ya kupashana taarifa za mradi na kushughulikia maswali
- Kumteua msimamizi wa mradi mwenye kujitoa kama mtu muhimu kwa ajili ya mawasiliano.
- Kuhakikisha kuwa tafsiri zinaendana na utamaduni na zinafaa kwa hadhira lengwa katika kila lugha

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu na uwezo wa kutoa huduma kwa mawanda yanayohitajika
- Wasifu wa Shirika unaoonyesha huduma zinazotolewa, uthibitisho wa utendaji, pampja na barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu wa awali.
- Leseni ya biashara
- Cheti cha usajili na ripoti ya sasa ya ukaguzi wa BRELA (ambatanisha nakala)
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka wa sasa
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Makampuni ya Ndani
- Wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika mradi, ikiwa ni pamoja na vyeti vyao, viwango vya elimu, uzoefu , na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho wa kutoa wa huduma za tafsiri kutoka kwa Bodi husika na mashirika yake kama vile Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi, na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga vita rushwa, ufisadi, na kulinda Haki za Binandamu.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo tarehe **11 March 2024** saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) au kabla ya tarehe hiyo. Kichwa cha Barua pepe kiwe: **00000481 Utoaji wa Huduma za Tafsiri.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na tangazo hili na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni ambazo zitakazojumuishwa kwenye orodha ya kwanza ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.




Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida, Kemirembe Lwota, akishiriki kutoa chanjo mwishoni mwa wiki wakati wa kampeni ya chanjo ya surua na rubella inayotolewa kwa watoto wenye umri kuanzia miezi 9 hadi miezi 59. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Bei sukari kubandikwa barabarani

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema taifa limeingia katika changamoto ya sukari lakini tatizo hilo ni la muda na litakwisha.

Amesema kuwa siku chache zijazo watatoa waraka wa kulazimisha kila mawakala na duka linalouza sukari liweke bei barabarani.

Bashe pia amesema taifa limelinda sekta ya sukari, akisisitiza wenye viwanda wanapolindwa, watambue wana wajibu kwa umma na uchumi wa taifa na si kuumiza wananchi.

Aliyasema hayo jana mkoani Tabora wakati wa uzinduzi wa ofisi mpya ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) iliyoanzishwa 2015 kwa lengo la kuleta mapinduzi ya kilimo kwa mipango endelevu inayokidhi mahitaji ya wakulima kupitia huduma tofauti za kifedha, kama mikopo ya moja kwa moja, yenye ushirika na dhamana.

"Kuna mtu juzi alileteva sukari hapa halafu anaweka faida ya Sh. 5,000 kwenye mfuko, hatuwezi kuruhusi hivi, lazima tufanye 'decentralization' ya mifumo ya usambazaji sukari, mtu wa Kigoma anafuata sukari Kahama au Mwanza si sawa.

"Lazima waweke mawakala katika mikoa, Coca-Cola kwani tunazifuata Dar es Salaam, si tunachukua kwenye 'depot' hapahapa Tabora! Kwanini isiwezekane kwenye sukari? Kwanini sekta ya sukari haiguswi, imefungwa fungwa kama kitu fulani kitakatifu? Bashe alihoji.

Alisema sekta hiyo inapewa mikopo kwa wakati na kwamba benki ya TADB iliipatia mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 70 kama sehemu ya utekelezaji wa uanzishwaji wake ambao ni kutoa huduma za kifedha kwa kupitia kongani na minyororo ya thamani kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kimkakati katika kilimo na kwa wakulima wadogo.

Waziri Bashe alisema yeye ni miongoni mwa wanaozisaidia sekta binafsi, lakini hawezi kufanya hivyo kwa zinazoumiza watu, akiwasisitiza kuwa waache kuhangaika na kama wana jambo, waende wizarani wakalijadili.

Alieleza kuwa haiwezekani kwa baadhi ya wafanyabiashara kupewa kibali cha kuingiza sukari tani 10,000 ilhali wanaishia kuleta tani 2,000 ambazo pia zinakuja kwa mafungu.

"Ninataka niwaambie Watanzania ukweli, wanataka tupate uhaba bei iende juu, wananchi waizoee bei ya Sh. 5,000, hata hali ikirekebishika tuendelee kuinunua kwa bei hiyo, haitowezekana, hatuwezi, tuwe waungwana, lazima tutende haki.

"Na mimi niwaambie mfumo wa kibepari wowote na kuna watu wanaleta hoja wanasema 'waziri kwanini unatoa bei elekezi', pale penye ukiritimba wa bei, serikali lazima isimamie.

"Mimi niwaambie tutasaidia viwanda vyetu, tutavilinda, lakini hatutaruhusu vichukue faida ya kuumiza wananchi kutokana na changamoto iliyojitokeza.

"Nimewaambia lazima wafungue maghala, wawe na mawakala kwenye mikoa, haiwezekani mtu anasafiri zaidi ya Km 700 kwenda kufuata sukari na kurudi, hatuwezi kuruhusu aina hii ya biashara, haiwezekani!" Bashe alisisitiza.

Alisema wameshagawana maeneo hivyo wanataka kuona yanakuwa na kituo cha mauzo, mawakala zaidi ya mmoja ili wananchi wapate huduma.

"Tumewaambia wenye viwanda tunawalinda, tunataka uwazi kwenye gharama za uzalishaji, unapolindwa na kutunzwa una haki, lakini vilevile una wajibu, lazima tujue gharama zako za uzalishaji, lazima watanzania wajue tunabadili mfumo ambao haujawahi kuguswa kwa miaka 30, 40.

"Ni ngumu kupambana, lakibi tutashinda kwa uwezo wa Mungu, tumetoa nafuu ya asilimia 53, lazima hiyo nafuu tuione kwa mlaji.

Rais katoa hiyo ili aipate mtanzania wa kawaida, sukari inakuja na itaendelea kuja hadi hali itakapokuwa sawa," alisema Bashe.

Benki ya TADB tangu kuanzishwa kwake, imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 284 kufadhili miradi ya kimkakati 71 na kunufaisha wakulima wadogo 1,049,370.

# Matukio migongano binadamu, wanyama nchini yafikia 2,817

**Na Waandishi Wetu**

MATUKIO ya migongano kati ya binadamu na wanyamapori yanazidi kuongezeka, yakifikia 2,817 mwaka 2022/23 kutoka 833 yaliyorekodiwa mwaka 2016/17 na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

Ofisa Uhifadhi Kitengo cha Operesheni na Udhibiti Wanyamapori Wakali na Waharibifu TAWA, Isack Chamba, alibainisha hayo kwa waandishi wa habari ambao ni wanachama wa Chama Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) mjini Bagamoyo, Pwani mwishoni mwa wiki.

Alisema migogoro hiyo ilianza kushika kasi mwaka 2018. kukiripotiwa matukio 1,519 na ndani ya miaka mitano yalifikia 2,817 sawa na ongezeko la asilimia 23.7 kwa mwaka.

Alisema migongano hiyo imekuwa na madhara makubwa kwa binadamu hasa katika sekta ya kilimo kwa kuwa utafiti wao unaonesha uharibifu wa mazao unaongezeka kwa asilimia 118 kwa mwaka, tembo wakiongoza kwa uvamizi huo kwa asilimia 80.

Ili kupunguza kasi ya migogoro hiyo, ofisa huyo alisema kuwa mwaka 2018, Wizara ya Maliasili na Utalii iliandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Migogoro Kati ya Binadamu na Wanyamapori (2020-2024) unaotumiwa kama mwongozo kwa wadau wote wa uhifadhi.

Alisema kuwa wakiwa sehemu ya wadau wanaotekeleza mikakati hiyo, wanatoa elimu kwa wanajiji ya ili wajue namna ya kuishi na wanyamapori kwa amani. Desemba mwaka jana walipeleka katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, vijana 120 wanaotoka kwenye vijiji vilivyoko kwenye shoroba za wanyamapori ili kupata mafunzo ya njia rafiki za kukabiliana na wanyamapori.

Alisema pia wanafanya doria za mara kwa mara katika vijiji ili kudhibiti wanyama wakali na waharibifu na mwaka 2022/23 walifanya jumla ya doria 18,894.

Alisema licha ya jitihada kubwa wanazofanya kukabiliana na migogoro hiyo kasi ya utekelezaji wao ni ndogo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa vitendea kazi na gharama kubwa za kuendesha operesheni ya kudhibiti wanyama.

Mtaalamu wa Migongano Kati ya Binadamu na Wanyamapori, John Noronha, alisema kwa kuwa migongano hiyo haiwezi kuisha kutokana na mwingiliano wa binadamu na wanyama, serikali na wadau hawana budi kutafuta njia nzuri ya kufanya binadamu na wanyama waishi kwa amani na kutumia rasilimali zilizopo pamoja.

Alisema kwa sasa usuluhishaji wa migogoro hiyo unaegemeza zaidi kwenye fedha za wafadhili na pale na zinapokwisha, hali inarudi kama zamani, hivyo kuna haja serikali na wadau wa uhifadhi kuja na njia endelevu za kukabiliana na hali hiyo.

Mshauri wa Mradi kutoka Shirika la Maendeleo ya Ujerumani (GIZ) Tanzania, Anna Kimambo alisema katika kuunga mkono jitihada za serikali za kupunguza migongano hiyo, wameungana na JET ili kutoa elimu kwa jamii zinazoishi kwenye shoroba kupitia kwa waandishi wa habari.

Alisema lengo kuongeza uelewa juu ya umuhimu wa binadamu na wanyama katika shoroba kuishi kwa amani ili iwe sehemu ya usuluhishi na si wachochezi wa migongano hiyo.

Jumla ya vijiji 30 katika Halmashauri za Liwale (Lindi), Namtumbo na Tunduru (Ruvuma) vinatarajiwa kufikiwa katika mradi huo.

Mkurugenzi wa JET John Chikomo alisema mafunzo hayo yataongeza uelewa kwa waandishi wa habari kuhusu migongano ya binadamu na wanyamapori, hivyo kuandika habari zenye kutoa suluhisho.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Maliasili na Utalii, John Mapepele, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ikiwamo GIZ na JET, wameweka nguvu ya kutumia njia bora ya kumaliza migongano hiyo ambayo imekuwa inaathiri pande zote mbili.

"Tumeona njia pekee ya kumaliza mgongano wa binadamu na wanayamapori ni kushirikisha wadau kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka hifadhi mbalimbali, wawe na uelewa mpana na si kuona wanyama kama ni maadui zao," alisema Mapepele.

Ofisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Michael Ngowi, alisema kunahitajika nguvu ya ziada kutoa elimu kwa jamii inayoishi jirani na hifadhi ili kuondokana na dhana potofu kuwa wanyamapori ni maadui kwao, kitu ambacho ni tofauti.

***Imeandaliwa na Jenifer Gilla na Ashton Balaigwa**

HABARI KITAIFA

# Majaliwa azindua redio ya halmashauri

Na Munir Shemweta, MLELE

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua kituo cha redio Mpimbwe FM kinachomilikiwa na Halmashauri ya Mpimbwe, wilayani Mlele, mkoani wa Katavi, akiagiza redio hiyo itumike kutangaza shughuli za maendeleo.

Uzinduzi huo ulifanyika jana katika halmashauri hiyo, Majaliwa akiwa mgeni rasmi kwenye mkutano huo huku Mbunge wa Kavuu, Geophrey Pinda akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha kuanzia Novemba 2020 hadi Februari 2024.

Majaliwa aliagiza redio hiyo kutoa nafasi kwa wakuu wa idara za Halmashauri ya Mpimbwe kuelezea kazi zinazofanywa na halmashauri hiyo sambamba na idara nyingine za serikali ili wananchi wafahamu.

"Unaweza kumwita mkuu wa idara ya elimu katika kipindi ili aeleze umuhimu wa masuala mbalimbali yanayofanywa katika sekta ya elimu kwenye jimbo la Kavuu pamoja na Halmashauri ya Mpimbwe kwa ujumla.


"Wananchi wanaweza kuitumia vizuri redio namna wanavyofurahishwa na kazi zinazofanyika na wakati huo wakuu wa idara wakaitumia kueleza mikakati iliyopo katika halmashauri hiyo kama vile masuala ya afya na elimu," Majaliwa alielekeza.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko alimweleza Waziri Mkuu kuwa kuzinduliwa kwa redio hiyo kunatoa fursa kwa wananchi wa halmashauri na maeneo jirani kupata taarifa za uhakika na kwa urahisi.

"Redio uliyoizindua ni ya kwanza kumilikiwa na taasisi ya serikali katika mkoa huu na ujio wa redio hii ni mkombozi kwa mkoa huo kwa kuwa itasaidia kufikisha ujumbe wa serikali kwa wananchi sambamba na kupokea kero na changamoto za wananchi," alisema Mwanamvua.

Mbunge wa Kavuu ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, alisema uzinduzi wa redio hiyo ni mkombozi kwa halmashauri na wananchi wa jimbo lake kwa kuwa watapata fursa ya kuitumia kwa maendeleo.

Alisema pamoja na mafanikio ya kuwa na kituo cha redio, kuna changamoto kadhaa kama vile halmashauri yake kuwa na upungufu mkubwa wa watumishi ambapo kwa sasa ina watumishi 892 tu sawa na asilimia 43 ya mahitaji.



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, akiwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Arusha Mount Meru, akimjulia hali mmoja wa majeruhi wa ajali iliyotokea mwishoni mwa wiki jijini Arusha iliyohusisha lori na magari mengine matatu na kusababisha vifo vya watu 25 na majeruhi 21. Habari Uk. 3. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Waziri aagiza kuondolewa waliovamia hifadhi misitu

Na Elizabeth Zaya

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Angella Kairuki, ameagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuwatoa haraka wananchi waliovamia katika maeneo mbalimbali ya hifadhi za misitu nchini.

Pia ameagiza hifadhi zote kufanyiwa doria ya kutosha ili kuhakikisha zinalindwa dhidi ya uhalifu na waharibifu ambao wamekuwa wakivamia mara kwa mara.

Aliagiza kuchukuliwa hatua hizo mwishoni mwa wiki alipokabidhi magari na pikipiki katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kuimarisha doria kwenye rasilimali za hifadhi za misitu na miti.

Waziri Angella alisema wizara itahakikisha inapambana kukomesha kila aina ya uhalifu kwenye rasilimali za misitu nchini.

"Kuna siku isiyo na jina, wakati wowote na mimi nitaingia msituni. Sasa nikute wachimbaji hawaeleweki, mifugo imeingizwa haieleweki, kwa kweli sitamvumilia mtu baada ya hapo, kitakachofuata ni hatua stahiki hapohapo," alionya.

Alitoa tahadhari kwa wavamizi na wahalifu ambao wamekuwa wanavamia askari kwenye hifadhi hizo na kuwajeruhi au kuhatarisha maisha yao. Serikali iko macho na itahakikisha inaweka mitego ya kuwanasa na kuwachukulia hatua.

Aliwataka wakuu wa kanda na wakuu wa hifadhi za misitu nchini kufanya alichokiita uamuzi mgumu kwa watumishi wao wanaokwenda kinyume cha maadili, itatulazimu sisi tuliopo huku wizarani kufanya uamuzi mgumu. Kwa hiyo, ninataka mchukue hatua stahiki na mnawajua.

"Msipochukua hatua dhidi ya wale wanaokwenda kinyume cha maadili, itatulazimu sisi tuliopo huku wizarani kufanya uamuzi mgumu. Kwa hiyo, ninataka mchukue hatua stahiki na mnawajua.

"Fuateni watu kule chini waliohujumiwa na watu wetu, tunafahamu majungu ya hapa na pale hayakosekani, lakini ninawasihi fuateni miongozo ya kazi mliyopewa, kila mtu kwa nafasi yake," aliagiza.

Alipongeza TFS kwa namna ambavyo imetatua migogoro iliyokuwapo kati yao na wananchi bila pande zote mbili kuathirika.

Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema vijiji 423 kati ya 438, vimeshapitiwa mipaka yake na kufanyiwa tathmini kwa ajili ya kuhamishwa.

Alitaja baadhi ya changamoto ambazo wanapambana nazo zinajumuisha wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu, uvunaji haramu wa misitu, uhalifu wa kutumia pikipiki na baiskeli kwa kusafirisha mazao kwa kutumia njia haramu pamoja na matukio ya moto.

# Makamu wa Rais aongoza maziko ya baba wa waziri

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameongoza wananchi katika maziko ya mwili wa Masauni Yussuf Masauni, baba wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Yussuf Hamad Masauni.

Mzee Masauni aliwahi kushika nafasi mbalimbali serikalini na ya mwisho alikuwa Kamishna wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar, akistaafu mwaka 1985.

Alifariki dunia mwishoni mwa wiki iliyopita katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikokuwa anapatiwa matibabu na kuzikwa juzi katika makaburi ya Mwanakwereke, visiwani Zanzibar.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi alifika eneo la Migombani, Wilaya ya mjini Unguja, nyumbani kwa Mzee Masauni kuipa pole familia na kuwataka kuwa na subira baada ya kumpoteza mzazi wao.

Dk. Mwinyi pia alisifu utumishi uliotukuka wa Mzee Masauni katika kipindi chote alichotoa huduma katika nyadhifa mbalimbali za utumishi wa umma.

"Ninatambua na kukumbuka nafasi na nyadhifa mbalimbali alizotumikia Mzee Masauni akiwa mtumishi wa umma, mchango wake ukiletea maendeleo nchi ya Zanzibar.

"Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania kwa ujumla, tumwombe Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, " aliomba Rais Mwinyi.

Akizungumza kwa niaba ya familia baada ya ibada ya maziko, msemaji wa familia, Abdallah Miraji Othman, alimshukuru Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, na viongozi mbalimbali akiwamo Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdula, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, Rais mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume na viongozi wengine kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiwamo mawaziri na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF simamieni kanuni hii, imejibu Simba, Yanga CAF

**MABINGWA** wa Tanzania Yanga wamefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakiwa na mchezo mmoja mkononi, tena wakiwa kundi lililoonekana gumu, ambalo lina Mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri, Medeama ya Ghana na CR Belouizdad ya Algeria ambayo juzi ilikubali kichapo cha mabao 4-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba nayo Ijumaa iliyopita, ikajiweka kwenye mazingira mazuri ya kutinga hatua hiyo, ilipolazimisha sare ugenini dhidi ya wenyeji wao, Asec Mimosas ambao ni vinara wa Kundi B.

Hivyo, matokeo ya timu hizo za Tanzania yanazifanya ziendelee kushika nafasi ya pili ya msimamo, Simba ikiwa Kundi B linazozijumuisha Asec Mimosas, Wydad Casablanca ya Morocco na Jwaneng Galaxy ya Botswana, ikiwa na pointi sita na Yanga Kundi D ikiwa na pointi nane.

Ukifuatilia vikosi vya timu hizo, ni kwamba kila kimoja kilikuwa na wachezaji watatu wa Kitanzania kati ya wale 11 walioanza. Simba ilikuwa na wazawa, Aishi Manula, Shomari Mapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala', na Yanga ilikuwa na Dickson Job, Mudathir Yahaya na Ibrahim Hamad 'Bacca.'

Wachezaji wanane kwa kila timu walioanza ni wa kigeni, ambao kwa kiasi kikubwa ndiyo wanaozibeba timu zetu za Tanzania kwa sasa. Timu hizo pia zilikuwa na wachezaji ambao hivi karibuni walikuwa wametoka kwenye vikosi mbalimbali vya timu zao za taifa kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika, AFCON.

Simba ilikuwa na wachezaji wanne waliokuwa AFCON ambao ni Manula, na Tshabalala waliokuwa wakiichezea Tanzania, Henock Inonga, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Clatous Chama, Zambia achilia mbali Mzamiru Yassin na Kibu Denis walianzia benchi.

Kwa upande wa Yanga ilikuwa na wachezaji watano ambao ni Djigui Diarra aliyekuwa na timu ya Mali, Stephane Aziz Ki na timu ya Burkina Faso, Kennedy Musonda wa Zambia, Bacca na Mudathir, Tanzania.

Katika hili, hatuwezi kuzipongeza timu hizo pekee, bila kuwapa kongole Bodi ya Ligi nchini (TPLB), chini ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kwa kuweka msisitizo ikiwamo kutengeneza kanuni ya kuzitaka klabu kusajili wachezaji bora wa kigeni na angalau waliowahi kucheza ama wanaocheza timu za taifa.

Kabla ya hili, timu zilikuwa zikisajili wachezaji kutoka nje ya nchi ambao walioonekana kuwa ni wa kuokoteza, lakini baada ya TFF na TPLB kuwa wakali, tumeona sasa wachezaji wanaokuja ni wale ambao wanazichezea timu zao za taifa, waliowahi kuzichezea, na wengine wanaitwa na kuchujwa.

Jambo hili limezifanya timu zetu kuwa na kiwango cha juu na kuzisumbua hata timu za Afrika Kaskazini maarufu kama 'Waarabu', ambazo miaka ya nyuma zilizifanya timu za Tanzania kama 'mwembe wao wa uani', lakini sasa zimekuwa na hofu zinapangwa nazo.


Kuwapo kwa wachezaji hao bora kumewaboresha hata wachezaji wa ndani kwani wamekuwa wakipambana ili kupata namba, jambo ambalo linaboresha viwango vyao kiasi cha kuifanya hata Timu ya Taifa ya Tanzania kwa sasa nayo kugeuka kuwa si mchekea tena.

Rai yetu kwa TFF na TPLB ni kuzidi kusimamia vema kanuni hiyo ya klabu za Ligi Kuu na Championship kusajili wachezaji wenye ubora zaidi ili kuja kuongeza ushindani kwa wazawa na hatimaye kuleta mafanikio ya soka nchini kama ambavyo tunaona kwa Simba na Yanga hata kwa Timu ya Taifa, Taifa Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Yanga, nafasi nusu fainali CAF ni kubwa

Na Adam Fungamwango

**HISTORIA** imeandikwa baada ya Yanga kufanikiwa kuingia hatua ya robo fainali kwa mara ya kwanza tangu mfumo wa sasa wa Ligi ya Mabingwa Afrika uanzishwe.

Yanga ilikuwa haijawahi kufanya hivyo, tangu ilipoanza kucheza ligi ya mfumo huo 1998 na kuishia hatua ya makundi.

Mfumo wa makundi ulianzishwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) 1997, ambapo kabla ya hapo timu zilikuwa zinacheza kwa kutoana kuanzia hatua ya awali hadi fainali.

Mfumo wa awali ulianzishwa mwaka 1964, na Yanga ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali mara mbili.

Yanga ilifanya hivyo kwa miaka miwili mfululizo, 1969 ilifanya hivyo kwa kuitoa Fitarikandro ya Madagascar jumla ya mabao 4-3, ilishinda 4-1 nyumbani, kabla ya kwenda kufunga mabao 2-0 na kutinga hatua hiyo, lakini kikwazo cha kuingia nusu fainali kilikuwa ni Asante Kotoko ya Ghana, ambapo baada ya sare ya bao 1-1 ugenini na kama hiyo nyumbani, ilitolewa kwa kanuni ya kurusha shilingi ili kumpata mshindi.

Ikumbukwe wakati huo kanuni ya kupigiana penalti tano-tano timu zikitoka sare ilikuwa bado haipo.

Mechi ya maamuzi ilifanyika hapa hapa nchini, Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru Dar es Salaam), ambapo ilishuhudia wageni shilingi ikianguka upande wao baada ya sare ya jumla, mabao 2-2 nyumbani na ugenini.

Kwa bahati nzuri, mwaka 1970, Yanga ilifanikiwa kutinga tena hatua ya robo fainali kwa kuitungua, Nakuru All Stars ya Kenya jumla ya mabao 3-2, kwani baada ya kufungwa bao 1-0 ugenini, ilishinda nyumbani mabao 3-1.

Bahati mbaya ikaja kwa kukutana na mpinzani yule yule wa msimu uliopita,

Asante Kotoko, safari hii ilianzia nyumbani na kupata sare ya bao 1-1 na kwenda kufungwa ugenini mabao 2-0 na kutolewa kwa jumla ya mabao 3-1 na ndiyo mwaka ambao Waghana hao walitwaa ubingwa wa Afrika.

**Bahati mbaya ikaja kwa kukutana na mpinzani yule yule wa msimu uliopita, Asante Kotoko, safari hii ilianzia nyumbani na kupata sare ya bao 1-1 na kwenda kufungwa ugenini mabao 2-0 na kutolewa kwa jumla ya mabao 3-1 na ndiyo mwaka ambao Waghana hao walitwaa ubingwa wa Afrika.**

Binafsi, niwapongeze viongozi, benchi la ufundi na wachezaji wa Yanga kwa kazi nzuri ya pamoja ambayo wameifanya ili kurudisha heshima ya klabu hiyo iliyokuwa nayo miaka hiyo.

Moyo wa kujituma na upambanaji wa wachezaji wa Yanga unaweza kabisa kuifanya timu hiyo kutinga hatua ya nusu fainali kama ilivyofanya Simba mwaka 1974.

Wakati Simba ikiishia robo fainali mara nne na hii inayokwenda inaweza kuwa ya tano, lakini bado wanachama na mashabiki hawana uhakika kama timu yao inaweza kumudu kuvuka na kucheza nusu fainali hata kama ikiingia robo, lakini si Yanga.

Kwa sasa ipo kwenye kiwango cha juu na inaweza kwenda nusu fainali kwa kukutana na timu yoyote ile ikapata ushindi.

Ni jambo la heshima kwa Ligi ya Tanzania na nchi kwa ujumla ambayo kwenye miaka ya katikati ya 1960, mwanzoni mwa miaka ya 1990 soka lilikuwa juu, lakini kuna sehemu ambayo kama nchi ilikwama.

Yanga inatoa ujumbe kwa timu zingine kuwa unapotengeneza kikosi bora, chenye wachezaji wenye viwango vya hali ya juu, basi unapata ushindi wowote, popote na kwa klabu yoyote ile Afrika.

Kwa miaka ya hivi karibuni kutokana na teknolojia ya kuonyeshwa kwa mechi, zile figisu ambazo tumekuwa tukizisikia kutoka kwa baadhi ya nchini uwanjani hazipo tena, ni soka tu linalotembea uwanjani, na timu yenye uwezo ndiyo inayoshinda.

Tumeanza kuona sasa kuwa timu inayojipanga vema inashinda popote pale. Hongereni Yanga kwa kufanikiwa kutinga hatua hiyo huku mkiwa pia na mchezo mmoja mkononi, kitu ambacho ni ngumu kwa timu nyingi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kufanya hivyo.

# Halmashauri zapewa mbinu kuepuka adha bomoabomoa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida ameelekeza halmashauri za mkoa huo zinapogawa viwanja kwa ajili ya makazi, zifikirie kuhusu mpango wa baadaye wa kujenga barabara ili kuepuka wananchi kubomolewa nyumba zao serikali inapoamua kujenga barabara na hivyo kusababisha migogoro isiyo ya lazima.

Peter Serukamba aliagiza hayo juzi baada ya kukagua barabara na madaraja yanayojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida na Manispaa ya Singida katika ziara yake ya kukagua miradi ya barabara katika wilaya zote za mkoa huo.

"Watu wa mipango miji kabla hatujagawa viwanja tuangalie na miaka mitatu au mitano mbele kama hizo sehemu baadaye kutajengwa barabara kubwa, tuchukue tahadhari kwamba hapa pasijengwe nyumba ili kulinda nyumba za watu kubomolewa," aliagiza.

Serukamba alisema Sheria ya Barabara ina nguvu kubwa kuwa kuwa inapofikia mtu amejenga kwenye hifadhi ya barabara, ni lazima nyumba yake ibomolewe - iwe atalipwa fidia au asilipwe, jambo ambalo linasababisha malalamiko ya wananchi, lakini maofisa mipango miji wangekuwa makini, wangeepusha hayo.

Alielekeza halmashauri zisiwe zinagawa viwanja kwenye maeneo hatarishi ambako mvua kubwa ikinyesha kunatokea mafuriko na hivyo kusababisha maafa kwa wananchi.

Serukamba pia aliagiza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) Mkoa wa Singida unapojenga barabara, ufikirie kujenga njia za watembea kwa miguu ili kuepusha ajali ambazo zimekuwa zinatokana na watu kutembea barabarani.

Vilevile, alishauri Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kuhakikisha makandarasi wanaopewa kazi ya kujenga barabara, wawe wanapanda na miti kando ya barabara ili kuwe mandhari mazuri ya miji.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Ibrahimu Kibasa, alisema katika barabara zinazojengwa Manispaa ya Singida wamefikiria kujenga na barabara ambazo zitatumiwa waendesha pikipiki (bodaboda) na bajaji.

Kibasa alisema mpango wa kujenga barabara za bodaboda na bajaji utasaidia kuepusha ajali. Maeneo ya miji zinakojengwa barabara kutawekwa taa ili kupendezesha mji.

Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu alisema manispaa hiyo kwa mwaka huu wa fedha imetenga Sh. milioni 85 kwa ajili ya kufungua barabara za mitaani kwa lengo la kuisaidia TARURA kuongeza mtandao wa barabara.

# Joto lazidi kupanda uchaguzi wa ACT

**Na Halfani Chusi**




ZIMEBAKI siku tisa kufanyika uchaguzi wa wajumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo Kanda ya Pwani, mgombea wa nafasi hiyo, Husna Sungura (pichani) anatamba akichaguliwa, atasaidia kukivusha chama kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Husna ambaye kwa sasa ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho Pwani, amesema atajikita zaidi kutetea wanawake ndani ya vikao vya chama.

Mgombea huyo alitamba kufanya hayo alipozungumzia vipaumbele vyake jijini Dar es Salaam jana iwapo atashinda katika nafasi hiyo.

"Nitazisema changamoto za wanawake Kanda ya Pwani katika vikao vya chama. Nitaimarisha ngome za wanawake mikoani na majimboni na kuibua hamasa kwa wanawake Kanda ya Pwani," alitamba Husna huku akiomba wajumbe wajitokeze kwa wingi kumpigia kura kumchagua.

Vipaumbele vyake vingine ni kukitetea na kukinadi chama kwa watanzania ili wavutiwe nacho na kujiunga, kuongeza ubunifu katika mipango itakayokipaisha chama kiuchumi na kisiasa na kuhakikisha falsafa ya chama inaeleweka kwa Watanzania.

Husna ambaye amekuwa mwanachama wa kawaida tangu mwaka 2015, ilipotimu mwaka 2019, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti Ngome ya Wanawake Pwani, nafasi aliyodumu nayo mpaka Januari mwaka huu .

"Niliukataa udiwani viti maalum mwaka 2015 nikiwa Kigoma baada ya kufanya kazi kubwa na kupata mbunge na madiwani ili nirudi Pwani, Dar es Salaam kuendelea kukieneza chama, wenye moyo kama huo ni wachache na nilifanya hivyo nikiwa mwanachama wa kawaida, sikuwa na cheo chochote," alisema Husna.




Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Makamba jijini Dar es Salaam wakiwa na bango lenye ujumbe baada ya kupata elimu kuhusu madhara ya rushwa ya ngono, iliyotolewa na Shirika la Usawa wa Kijinsia Tanzania (SUKITA), mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri: TASAF izipe kipaumbele kaya zenye watu wenye ulemavu

**Na Lusungu Helela**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameutaka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuweka nguvu zaidi katika kuingiza kaya maskini zenye watu wenye ulemavu kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ili nao wajiinue kiuchumi.

Simbachawene aliagiza hayo jana alipotembelea na kukagua utekelezaji miradi ya TASAF katika Kijiji cha Kinywang'anga, Wilaya ya Iringa, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi mkoani humo kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa na TASAF.

Alisema TASAF imekuwa mkombozi kwa wananchi wanaonufaika kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na mpango huo huku akisisitiza kuwa katika awamu ijayo iwaangalie zaidi watu wenye ulemavu kwa kuwa wamekuwa wanakosa fursa nyingi kulingana na changamoto walizokuwa nazo.

"Kaya zenye watu wenye ulemavu na hazijiwezi kimaisha, zina mzigo mara mbili kulinganisha na kaya zisizojiweza na hazina watu wenye ulemavu, hivyo ni lazima kaya zenye walemavu zipewe kipaumbele zaidi. Alisema moja ya dhamira za serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kaya maskini zenye watu wenye ulemavu zinapata uhakika wa milo mitatu kama zilivyo kaya nyingine maskini.

Waziri Simbachawene alisema serikali inafanya kazi kubwa kuhakikisha fedha zinazotoka zinafika kila mahali na kwa walengwa sahihi hasa wanaoishi vijijini katika kuboresha maisha ya Watanzania kupitia miradi mbalimbali ukiwamo wa TASAF.

Alisema miradi inayotekelezwa na TASAF inagusa maisha ya wananchi moja kwa moja na kushirikisha jamii katika uhalisia wake, akisema huo ndio msingi wa viongozi wa Tanzania.


"Lengo la miradi ya TASAF ni kuondoa umaskini wa kipato kwa mtu mmoja mmoja na kaya, ndio maana kuna wanufaika wanaopewa fedha za moja kwa moja ili kuwapa ahueni katika hali zao za maisha," alisema Simbachawene.

Katika ziara hiyo, Waziri Simbachawene alitembelea mradi wa ujenzi wa birika la kunyweshea mifugo katika Kijiji cha Kinywanga'nga, akiguswa na utekelezaji mradi huo ambao unakwenda kuinua sekta ya uvuvi na kugusa moja kwa moja maisha ya wafugaji.

Meneja wa Miradi ya Ajira za Muda Mfupi TASAF, Paul Kijazi, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ina afua tatu katika jamii, ikiwamo kuhawilisha fedha inayotolewa kwa wananchi wa kaya zisizokuwa na uwezo wa kufanya kazi wakiwamo wazee.

"Katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa tuna vijiji 134, vyote vinahawilishiwa fedha, tumeshaleta Sh. bilioni 3.663 katika awamu ya pili ya TASAF kwa walengwa, lakini pia tulileta fedha Sh. bilioni 1.09 kwa ajili ya vifaa vilivyotumika katika ajira za muda mfupi.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Ridhiwani: Haipendezi mwanafunzi kufeli shuleni, kuendesha bodaboda

**Na Julieth Mkireri,**
BAGAMOYO

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema maboresho yanayofanyika katika sekta ya elimu yanalenga kuhakikisha elimu bora inapatikana na ufaulu unaongezeka na si kuzalisha vijana ambao hawataleta mabadiliko ya maendeleo kwenye maeneo yao.

Amesema hafurahii kuona mwanafunzi anafeli shuleni kisha kujiunga mtaani kuendesha pikipiki za kusafirisha abiria, maarufu bodaboda.

Ridhiwani ambaye ni Mbunge wa Chalinze alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa katika Shule ya Sekondari Mboga kulikofanyika makabidhiano ya vifaa vya mradi wa maabara za kompyuta kwa shule nne za sekondari za Halmashauri ya Chalinze, wilayani Bagamoyo.

Katika makabidhiano ya vifaa hivyo vilivyotolewa na shirika lisilo la kiserikali la Reneal International Education Outreach, Naibu Waziri huyo alisisitiza wanafunzi kujikita kwenye masomo na kuachana na tamaa ambazo zinarudisha nyuma maendeleo.

"Wapo waliotangulia kuolewa kabla ya muda, angalieni maisha yao yalivyo duni, achaneni na makundi ambayo hayana tija kwenu, sikubali kuona mnafeli na kwenda kuendesha bodaboda wakati mazingira ya elimu yameboreshwa kwa asilimia kubwa," alisisitiza.

Alisema awali shule za kata zilikuwa nyuma kwenye upande wa TEHAMA, lakini sasa maboresho yanaendelea kuhakikisha wanafunzi wanajifunza somo hilo na kwenda na teknolojia ya sasa.

Alikemea tabia ya baadhi ya wazazi kushawishi watoto wao kufeli kwenye mitihani yao ya kitaifa Ili wasiendelee na masomo, wakidai kukwepa gharama, jambo ambalo si sahihi kwa kuwa tayari serikali imeondoa ada shuleni.

Ridhiwani alishukuru shirika hilo kwa kuwezesha kompyuta hizo ambazo zitasaidia wanafunzi kuondokana na kutafuta vitu vingi maktaba ambavyo watavipata kwa urahisi kwenye kompyuta.

Awali Ofisa Elimu Sekondari, Salama Ndyetabura, alielekeza walimu na wanafunzi kutunza vifaa hivyo ili viwe na manufaa kwa vizazi vya sasa na baadaye.

Alisema halmashauri hiyo ina shule za sekondari 26, nne pekee ndizo zimenufaika na msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 71.1. Hizo ni Shule za Saekondari Mboga, Msata, Mdaula na Mandera. Lengo ni kusaidia ujifunzaji na ufundishaji masomo, hususani ya sayansi.

Alimshukuru mbunge huyo kwa kufanikisha upatikanaji vifaa hivyo ambavyo vinakwenda kurahisisha ujifunzaji masomo ya sayansi kwa vitendo kupitia kompyuta, walimu kuandaa masomo na matokeo kwa wakati na kuibua na kumkuza vipawa vya wanafunzi katika matumizi na maendeleo ya teknolojia.

Ofisa TEHAMA Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambaye ni mratibu wa shirika lililotoa msaada huo, alisema mbunge wa jimbo hilo aliomba kompyuta kwa shule zote za sekondari za jimbo hilo na kwa kuanzia wametoa kompyuta 20.



Balozi John Ulanga, Mkurugenzi wa Biashara ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (kushoto), akimkabidhi cheti Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja wa Benki ya NMB, Abella Tarimo (wa pili kushoto), wakati wa hafla ya utoaji tuzo za Annual Tanzania Service Excellence Awards 2024 jijini Dar es Salaam, benki hiyo ilinyakua jumla ya tuzo tatu. Katikati ni Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yang'ara katika Tuzo za Mwaka za Ubora wa Huduma

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeshinda tuzo tatu katika Tuzo za Mwaka za Ubora wa Huduma Tanzania (Annual Tanzania Service Excellence Awards) 2024 zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, huku ikitangazwa mshindi wa jumla wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) katika kampuni zinazofanya kazi nchini.

Benki hiyo pia imeibuka mshindi wa pili katika sekta ya kibenki na mshindi wa pili katika kipengele cha mpango maalum na ujumuishi wa huduma kwa wateja.

Tuzo hizo zilizoandaliwa na Taasisi ya Chartered Institute of Customer Management zilitambua dhamira ya Benki ya NMB katika utoaji huduma bora na kubadilisha maisha ya watu kwa kutoa huduma wezeshi kijamii na kiuchumi.

Tuzo za Service Excellence Awards zilianzishwa mnamo mwaka 2010 na zimekuwa zinafanyika katika nchi mbalimbali barani Afrika, lakini zimefanyika kwa mara ya kwanza nchini mwaka huu. Akizungumza baada ya kupokea tuzo hizo, Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja wa Benki ya NMB, Abella Tarimo, alisema tuzo hizo ni uthibitisho wa utekelezaji mzuri wa mkakati wa benki hiyo.

"Katika Benki ya NMB, kuridhika kwa mteja ndio msingi wa shughuli zetu ndiyo maana huwa tunamtanguliza mteja wetu. Tuliboresha mifumo yetu mwaka jana ili kuhakikisha kuwa tunatoa huduma bila changamoto.

"Kituo chetu cha huduma kwa wateja sasa kinafanya kazi saa 24 tangu Januari mwaka huu na yote haya yanaonesha jinsi gani tumejizatiti katika kuendelea kumpa huduma mteja wetu.

"Kupitia ubunifu wetu wa masuluhisho ya kidijitali, mtandao mpana wa matawi na wafanyakazi wanaojitolea, tutaendelea kuchangia katika ukuaji wa sekta ya fedha nchini na kutoa huduma za kipekee kwa wateja wetu pamoja na kuendeleza utekelezaji mkakati wa benki wa Uwajibikaji Kwa Jamii (CSI)," alitamba.

Balozi John Ulanga, Mkurugenzi wa Biashara ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, alisema muundo wa uchumi wa Tanzania umebadilika kwa kiasi kubwa miaka 30 iliyopita.

"Miaka 30 iliyopita, asilimia 48 hadi 50 ya Pato la Taifa (GDP) ilichangiwa na kilimo na sekta ya huduma ilichangia karibu asilimia 25 tu. Leo, karibu asilimia 50 ya Pato la Taifa inachangiwa na sekta ya huduma.

"Katika muundo sahihi wa nchi ya kipato cha kati, asilimia 50 ya Pato la Taifa kuchangiwa na sekta ya huduma, asilimia 20 au chini ya kuchangiwa na kilimo na asilimia 30 iliyobaki inachangiwa na sekta ya uzalishaji na nyinginezo," alifafanua. Ulanga wakati wa hafla hiyo alizitaka kampuni kuwekeza katika teknolojia ili kuboresha huduma kwa wateja huku akisisitiza kuwa uwekezaji katika teknolojia unarahisisha utendaji kazi.

"Huduma bora inatofautisha kampuni moja na nyingine. Wakati ni sasa kwa kampuni kuangazia jinsi zinavyoweza kuongeza utoaji huduma bora kwa wateja," alisema.

# Marekani na Tanzania kuendeleza ushirikiano wao wa kiuchumi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI ya Tanzania imeahidi kuendelea kushirikiana na Marekani katika kukuza biashara na uwekezaji ili kuchangia ukuaji uchumi wa Tanzania na Marekani.

Vilevile, Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na Chemba ya Wafanyabiashara wa Marekani-Tanzania (AMCHAMTZ) na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) ili kufanikisha malengo ya Mpango Mkakati wa AMCHAMTZ.

Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Sempeho Manongi aliyasema hayo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hashil Abdallah, wakati wa uzinduzi wa Mpango Mkakati wa AMCHAMTZ ya mwaka 2024.

Manongi alisema mpango mkakati huo unaolenga kuimarisha biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani ni hatua muhimu katika utekelezaji wa makubaliano ya "U.S.-Tanzania Commercial Dialogue" yaliyofikiwa na mawaziri wa biashara wa nchi hizo mbili.

Alibainisha kuwa mpango huo unalenga kushughulikia vikwazo vya biashara, kuboresha sera na kuongeza uwekezaji katika sekta muhimu kama vile nguo, ufundi, usindikaji chakula na ngozi.

Mwenyekiti wa AMCHAMTZ, Geofrey Mchangila, alisema unalenga kuimarisha uwezo wa wafanyabiashara wa Tanzania, kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza ufikiaji masoko ya Marekani.

Uzinduzi wa mpango huo wa AMCHAMTZ unatarajiwa kuchochea ukuaji biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani na hivyo kuongeza ajira na kuboresha maisha ya wananchi wa nchi hizo mbili.



# Watoto 738 Simanjiro wabainika na udumavu

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

WATOTO 738 wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wamebainika kupata tatizo la udumavu, licha ya kuwapo mkakati wa serikali wa kuendesha kampeni ya lishe katika eneo hilo.

Idadi hiyo ambayo ni sawa na asilimia 38 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wamegunduliwa katika kipindi kisichozidi miezi sita.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Ibrahim Yeo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza katika kikao cha mapitio ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) cha robo ya pili (Julai hadi Desemba) mwaka jana. Alisema tatizo hilo la udumavu linaathiri kwa kiwango kikubwa uwezo wa watoto hao kufundishika watakapofikisha umri wa kuanza shule.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023, umri wa mtoto kuanza darasa la kwanza ni miaka mitano.

"Chanzo cha watoto hao kudumaa ni wazazi kuona ni gharama kutengeneza chakula dawa ili kukabiliana na utapiamlo. Sasa ili kukabiliana na ukubwa wa tatizo hilo, serikali tumeanzisha utaratibu wa kutembea kata kwa kata kutoa elimu ya lishe kwa wazazi," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu tatizo hilo, Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Eshimuni Swai, alisema kati ya watoto hao waliogundulika kudumaa, watoto 44 pekee ndio walipelekwa hospitali na wazazi wao ili wapatiwe tiba.

"Wazazi wengine, waliishia kutoa sababu nyingi na kuona wanasumbuliwa ila kwa taarifa za idara ya afya, watoto 44 waliopelekwa hospitali wanaendelea vizuri," alisema Swai.

Kwa mujibu wa ofisa lishe huyo, kikwazo kiko zaidi kwa jamii ya wakazi wa Simanjiro, ambao idadi kubwa ni jamii za kifugaji zinazoamini mila na desturi potofu.

Kutokana na tishio hilo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Maryam Muhaji, ameagiza maofisa lishe, ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii mkoani hapa kuondoka ofisini na kwenda mitaani kuzungumza na wazazi, walezi kuhusu umuhimu wa lishe bora.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Obinna Anyalebechi, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Msasani mjini Moshi mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki, wakati wa uzinduzi ya programu iitwayo SMASHED inayolenga kuwafundisha wanafunzi dhidi ya madhara ya matumizi ya pombe kwenye umri mdogo. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Magori na kulia ni Mkuu wa shule hiyo, Hassan Daudi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tatizo uhaba wa vifaa kuhifadhi sampuli damu lapatiwa ufumbuzi

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI ya Marekani na Shirika la Tanzania Health Promotion Support (THPS), zimejitosa kumaliza tatizo la uhaba wa vifaa vya kusambaza na kuhifadhi sampuli za damu kwa wagongwa wa kifua kikuu na Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Tayari wabia hao wa maendeleo nchini wamepeleka vifaa hivyo katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 800, ambavyo vitatumiwa katika vituo vyote vilivyoko maeneo ya pembezoni mwa mji.

Jana Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema vifaa hivyo vitatumiwa na Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa (CDC), kwa ajili ya wenye maambukizi ya VVU na kifua kikuu.

Waziri Ummy alisema: "Serikali ya Marekani, kupitia Shirika la THPS, imeweka nguvu kubwa kwenye mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kutumia mbinu mbalimbali.

"Lengo kubwa ni kudhibiti maambukizi mapya, kuibua wote wenye maambukizi na kuwapatia matibabu waimarike na wafikie kiwango cha kufubaza virusi ili waweze kuishi maisha yao ya kawaida na kujenga uchumi.

...Napenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote kwenye sekta ya afya wanaounga mkono juhudi za serikali kwenye mapambano dhidi ya UKIMWI, tunaomba mwendelee na juhudi hizi na sisi tuko tayari kuwapa ushirikiano wa kutosha."

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la THPS, Dk. Redempta Mbatia, alisema mbali na kutoa msaada huo pia wanatengeneza mpango kazi wa bajeti ya zaidi ya Sh. bilioni sita ambazo zitatumika kugharamia utoaji wa huduma za kinga, matunzo na matibabu kwa Mkoa wa Tanga kwa mwaka wa kwanza wa fedha.

Zaidi alieleza: "Pia tumetenga Sh. bilioni 4.886 ambazo zitatumika moja kwa moja mkoani hapa (Tanga), kwa ajili ya kugharamia vipaumbele vyake, ikiwamo kuajiri watumishi wa huduma za afya".

Vifaa vilivyotolewa na wabia hao ni pikipiki 50, majokofu 72 ya kuhifadhia sampuli katika vituo vya afya, centrifuges 56 za kuchakata sampuli hizo, kompyuta 50, UPS 50 na printa 50.

"Huu ni mchango wa wa walipakodi wa Marekani, ambao wamejitolea ili kuwezesha utoaji huduma bora katika nchi yetu, kudhibiti na kuokoa maisha ya Watanzania.

"Wito wetu ni kwa watendaji watakaovisimamia, wavitunze ikiwamo kuvifanyia matengenezo kinga kwa wakati na tunaahidi kuendelea kushirikiana bega kwa bega katika kuunga mkono juhudi za serikali," alisema.

Akizungumzia msaada huo, Mkurugenzi wa Mradi wa Kituo cha Marekani cha Kuzuia na Kuzuia na Magonjwa (CDC), Dk. George Mgomella, alisema vifaa hivyo vimegarimu Sh. milioni 800.

# Serikali yabariki kampeni kupambana na ulevi shuleni

**Na Godfrey Mushi,**
MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema serikali imeridhia kuanzishwa kwa kampeni maalum ya kukabiliana na ulevi kwa wanafunzi wa shule za sekondari katika Wilaya ya Moshi, baada ya utafiti kuonyesha kuna waathirika wengi ni kuanzia miaka 15.

Kampeni hiyo inatokana na utafiti uliofanywa mwaka 2019 katika mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro, kubaini matumizi ya pombe kwa wanafunzi wa shule za sekondari wenye umri wa miaka 15 na zaidi.

Utafiti huo ulionyesha kiwango hicho cha matumizi ya pombe kwa wasichana kilikuwa ni asilimia 12.9 kwa Mkoa wa Mwanza na asilimia 63.9 kwa wavulana mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza kabla ya kuzindua kampeni hiyo, Babu alisema uamuzi huo unalenga zaidi kulinda ustawi na mustakabali wa kizazi cha vijana wa kitanzania.

Babu, aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori.

Kwa mujibu wa mkuu huyo, programu hiyo inatumia tasnia ya uigizaji ili kutoa elimu kuhusu matumizi ya pombe chini ya umri na athari zake hasi kwa vijana walioko shuleni.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika ambako vijana wengi huanza matumizi ya pombe mapema katika umri mdogo.

Kampeni hiyo imepewa jina la SMASHED, ilizinduliwa mwishoni mwa wiki katika Shule ya Sekondari ya Msasani.

Alisema wakati wa utafiti huo, imebainika kiwango cha matumizi ya pombe miongoni mwa wanafunzi wenye umri wa miaka 13 hadi 15 katika Mkoa wa Dar es Salaam, kilikuwa asilimia 5.6.





# Kanisa la EAGT Jerusalemu lafungwa kisa malumbano

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAMATI ya Ulinzi ya Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, imelazimika kulifunga Kanisa la EAGT Jerusalemu lililopo Kata ya Majengo Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kwa muda usiojulikana, baada ya kuibuka kwa mzozo wa umiliki baina ya mchungaji, waumini na viongozi wa jimbo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, akiongea na Nipashe alisema wamefikia maamuzi hayo baada ya kuibuka kwa mgogoro mkubwa baina ya mchungaji wa kanisa hilo, Dk. Felix Gwamiye, waumini wake pamoja na viongozi wa jimbo hilo ambao wanamtuhumu kwenda kinyume na miongozo ya kanisa.

Alisema wamelazimika kulifunga kanisa hilo ili kulinda amani ambayo ingeweza kuvurugika kutokana na kuwepo kwa viashiria vya vurugu kutoka makundi mawili ya waumini wa kanisa hilo wanaomfuata mchungaji Dk. Gwamiye na baadhi wanaofuata viongozi wa jimbo.

"Kwa mujibu wa mchungaji wa kanisa hilo, Dk. Gwamiye alihama EAGT Jerusalemu na kuhamia AGGCI tangu mwaka 2020 hatua iliyowaibua viongozi wa jimbo kutaka kumuondoa kwenye kanisa hilo na kumuweka mtu mwingine aweze kulihudumu," alisema Mhita.

Katibu wa jimbo hilo, Godfrey Justini, alitaja sababu sita ambazo zimesababisha kutaka kumwondoa mchungaji huyo kuwa ni pamoja na utovu wa nidhamu kwa viongozi wake wa jimbo, kanda na taifa kwa kukaidi maagizo ambayo yamekuwa yakitolewa na viongozi.

Sababu nyingine ni kuwa na kusudio baya la kubadilisha kanisa kutoka jina la awali la EAGT na kuwa kanisa jipya la AGGCI kinyume na sheria zao, kuondoa mabango na jiwe la msingi lililowekwa na Askofu Mkuu pasipo viongozi wa jimbo kufahamu au kujulishwa.

Alitaja sababu nyingine ni kujimilikisha mali za kanisa kinyume na sheria licha ya kuwa na mali zake binafasi kama vile shule na nyingine, huku akijipandisha cheo asichostahili kwa kujiita Askofu.

Naye Mchungaji Dk. Gwamiye alipoulizwa juu ya tuhuma hizo alisema, mpasuko wa Kanisa la EAGT ulitokea baada ya aliyekuwa Askofu Mkuu, Moses Kolola kufariki na kuibuka kwa kanisa jipya la AGGCI ambalo ndiyo wengi wameelekea huko baada ya kuwapo kwa misiguano ya muda mrefu katika kanisa hilo.

Hivyo, aliiomba serikali kuwafungulia kanisa ili waendelee na ibada, huku shauri likiwa linashughulikiwa kisheria, kwamba anazaidi ya waumini 800 na hivi karibuni walisalia nyumbani kwake sehemu ambayo siyo mahususi kwa ibada.



Ofisa Mthibiti kutoka Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Zera Mwankemwa, akitoa mafunzo kwa baadhi ya waandishi wa habari mkoani Shinyanga juzi, kufahamu majukumu ya taasisi hiyo, pamoja kutumia kalamu zao kuelimisha wakulima umuhimu wa matumizi ya mbegu bora za kilimo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kaya 65,627 zapewa vyandarua kujikinga na malaria Maswa

**Na Alex Sayi,** MASWA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu inatarajia kugawa vyandarua kwa kaya 65,627 ambazo zimeandikishwa wilayani hapa.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa Malaria wilayani hapa, Dk. Menancy Kikungwe, wakati akizungumza na Nipasha juu ya hatua zinazochukuliwa na halmashauri hiyo baada ya kutajwa kuwa na ongezeko la maambukizi ya vimelea vya ugonjwa wa malaria kwa asilimia 21.8.

Dk. Kikungwe alisema hadi kufikia Februari, 21 mwaka huu kaya zipatazo 65,627 zimeshaandikishwa, kwamba walilenga kuandikisha wananchi 427,864 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Alisema kazi ya uandikishaji ilianza Februari 05 mwaka huu na kumalizika Februari 23 ikijumuisha vijiji 120 kwa lengo la kugawa vyandarua 26,939 ili kukabiliana na maambukizi mapya ya ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya mwaka 2022 Wilaya ya Maswa ilikuwa na ongezeko kubwa la maambukizi ya vimelea vya ugonjwa wa malaria kwa asilimia 21.8, kwamba mkoa wote ulibainika kuwa na ongezeko la asilimia 11.

Pia ilibainika kuwa Wilaya ya Busega ilifuata kwa maambukizi iliyokuwa na ongezeko la asilimia 17, Bariadi Vijijini asilimia 18. Aidha, ongezeko hilo linatajwa kuwa kubwa wilayani hapa ikilinganishwa na utafiti uliofanyika mwaka 2017, ambapo maambukizi yalikuwa ni asilimia tano pekee.

Kadhalika, takwimu hizo zinaonyesha kuwa vifo vilivyotokana na ugonjwa wa malaria mwaka 2022 vilikuwa ni 11 huku, wastani wa wagonjwa wenye vimelea kwa Aprili na Juni kila mwaka ni 2,000, maambukizi yakiongezeka kwa wastani wa wagonjwa 400 hadi 600.

Mkazi wa Kata ya Sola wilayani hapa, Joseph Jilala alisema hatua ya ugawaji wa vyandarua itakuwa msaada katika kukabiliana na ugonjwa huo, kwani kwa sasa hali ya maisha imekuwa ngumu na kusababisha wananchi kushindwa kumudu kununua chandarua.

Jilala alisema: "Maisha ni magumu, sukari, nauli imepanda, umeme hatuna pamoja na mambo mengine yamefanya maisha yanakuwa juu, hivyo kwa hali hii hatuwezi kumudu hata kununua hicho chandarua".

# RC awatoa hofu waandishi upatikanaji wa habari

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla amewatoa hofu waandishi wa habari mkoani hapa juu ya uharaka wa upatikanaji wa habari kupitia ofisi yake.

Amesema ofisi hiyo itaendelea kushirikiana nao kwenye kuhabarisha umma kwa kupata taarifa sahihi kwa wakati na kwa uhakika.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa katika kikao kilicholenga kutambua mchango wa vyombo vya habari kwa maendeleo ya mkoa na taifa.


Alisema wanahabari mkoani hapa wamekuwa ni kiungo cha kuwafikia wananchi na kutatua adha wanazokumbana nazo, hivyo kuwataka kuendeleza ushirikiano na umoja huo ili kuifanya Mwanza kukua zaidi kiuchumi na kijamii pia.

"Mwanza ni mkoa wa pili kwa idadi ya watu na kwa kuchangia pato la taifa, lakini mimi nikiwepo hapa mwelekeo wangu ni kufanya uwe mkoa wa kwanza, sio wa pili katika kuchangia pato la taifa na tuifanye kuwa kitovu kwa Kanda ya Ziwa na nchi jirani," alisema Makalla.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC), Edwin Soko, alizisihi taasisi na mamlaka zote za serikali mkoani hapa kuhakikisha wanazingatia usalama wa waandishi wa habari wakati wote wanapofanya shughuli za uhabarishaji umma na kutowazungusha waandishi mara wanapohitaji taarifa.

Alisema waandishi wa habari mkoani hapa wapo kwa ajili ya kuhabarisha umma na kusaidia kupatikana kwa majawabu ya kero mbalimbali kwa jamii jambo ambalo wanafanya kwa weledi na kwa kuzingatia maadili ya uandishi.

Nipashe Spotika



ALONSO UKURASA 12-13



SALAH

# NYOTA WA5 WATAKAOTIKISA USAJILI MAJIRA YA JOTO 2024

**LONDON,** England

MUDA si mrefu sasa sarakasi za dirisha la uhamisho wa majira ya joto zitaanza. Baada ya Januari fupi ya kubana mikoba, soko linatazamiwa kulipuka msimu huu wa majira ya joto huku miamba wa Ulaya wakirejea kwenye matumizi yao ya kupita kiasi.

Tayari kuna tetesi nyingi zinazozunguka kuhusu uwezekano wa mikataba ya majira ya joto, lakini uhamisho si rahisi siku hizi, huku kukiwa na vuta nikuvute hadharani kwa wachezaji wanaotegemewa zaidi duniani.

Huku kukiwa na habari nyingi ambazo tayari zimejaa safu za magazeti, hebu tuangalie sajili tano ambazo huenda zikatikisa msimu huu wa joto, haya sasa...

**#1. Mohamed Salah**

Mustakabali wa Liverpool wa Mohamed Salah bado haujulikani, licha ya kwamba Mmisri huyo amekuwa katika kiwango bora tena msimu huu. 'Wekundu' hao watakuwa na nia ya kumbakisha supastaa wao mwenye umri wa miaka 31, pale Anfield, lakini mkataba wake unatamatika mwaka 2025 na mazungumzo juu ya kupewa mpya hayajafikia tamati kwa njia moja au nyingine.

Si siri kuwa Saudi Arabia wanatamani sana kumsajili mshambuliaji huyo na walikuwa tayari kutoa zaidi ya pauni milioni 150 hadi 200 kwa ajili yake msimu uliopita wa majira ya joto. Liverpool walipinga ombi la kutaka kumuuza Salah, lakini Ligi Kuu ya Saudia itarejea kwake katika dirisha lijalo la uhamisho, hiyo ni hakika.

Huku kukiwa hakuna mkataba mpya na Jurgen Klopp akiwa ametangaza kuondoka mwishoni mwa msimu huu, je Salah anaweza kumfuata kocha huyo mwenye umri wa miaka 56 nje ya mlango wa kutokea?

**#2. Victor Osimhen**

Victor Osimhen amekuwa akivutia sana pale Napoli tangu ahamie mwaka 2020 na hata alisaidia kuiongoza klabu hiyo kutwaa taji lao la kwanza la Serie A katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita. Mshambuliaji huyo wa Nigeria amekuwa mkali mbele ya lango, lakini uhusiano wake na waajiri wake uko mbali sana.

Rais wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, amethibitisha kwamba Osimhen huenda akaondoka hapo Naples msimu huu wa majira ya joto, huku uvumi ukidai huenda akahamia Ligi Kuu England. Chelsea ni miongoni mwa wanaotajwa kuwa na nia kubwa, huku klabu kama Paris Saint-Germain na Real Madrid pia zikimsaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

Huku Mwanasoka Bora huyo wa Afrika wa 2023, akitarajiwa kugharimu zaidi ya pauni milioni 100, linaweza kuwa sakata kubwa na msimu huu wa majira ya joto huku klabu zikipigania saini yake.

**#3. Rafael Leao**

Rafael Leao ameibuka na kuwa mmoja wa mawinga wasumbufu zaidi barani Ulaya katika miaka ya hivi karibuni akiwa AC Milan, huku ustadi wake ukiwa umemtahadharisha kwa timu nyingine za Ulaya. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno alikuwa akiwindwa sana na Chelsea msimu uliopita wa majira ya joto na kuna uwezekano akawa anayewavutia tena mwaka huu.

Paris Saint-Germain wanaripotiwa kumtazama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala kamili wa Kylian Mbappe na wana uwezekano wa kutumia nguvu zao za kifedha kumshawishi mshambuliaji huyo kuhamia Mji Mkuu wa Ufaransa. Milan wana vita ya kweli mikononi mwao kumbakisha Italia.

**#4. Jadon Sancho**

Ugomvi wa Jadon Sancho hadharani na Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, ulisababisha winga huyo wa England ambaye amepata taabu sana kufanya vema Old Trafford, kurejea Borussia Dortmund kwa mkopo Januari.

Hata hivyo, inasemekana hakuna chaguo katika mkataba wa mkopo wa Sancho ambao unaruhusu Dortmund kumsajili moja kwa moja, hiyo inamaanisha kwamba mustakabali wake utakuwa hewani tena msimu huu wa majira ya joto. Iwapo 'Mashetani Wekundu' wanataka tu kulinda thamani yake kabla ya kumsogeza kwenye dirisha lijalo bado haijafahamika, lakini siku zake zinaonekana kuhesabika kule Manchester.

**#5.Frenkie de Jong**

Dirisha la usajili halipitiki siku hizi bila ya Frenkie de Jong kutajwa kuondoka Barcelona, licha ya Mholanzi huyo kuendelea kusisitiza kwamba ana furaha kucheza hapo Katalunya. Lakini, bila kujali kukatishwa tamaa kwa kiungo huyo na uvumi wa mara kwa mara kuhusu mustakabali wake, mambo yanaendelea kwenye Ligi Kuu England.

Manchester United wanajulikana kuwa wanamwania kwa muda mrefu, na Ten Hag anasemekana kutaka kufanya kazi na De Jong tena baada ya uchezaji wao wa kuvutia huko Ajax pamoja. Hata hivyo, Chelsea pia wana nia ya kuongeza jina lingine ghali kwenye safu yao ya kiungo msimu huu wa majira ya joto kwa kumwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26.

## ISIKUPITE

BUKAYO Saka amefunga katika mechi tano mfululizo za ligi kwa mara ya kwanza katika maisha yake ya soka. Idadi hiyo inamfanya kuwa mchezaji wa kwanza wa Uingereza kufunga katika mechi tano mfululizo za Ligi Kuu akiwa na Arsenal tangu Ian Wright (alipofunga mabao saba kati ya Septemba na Novemba 1994).



## Extra Time




# MAKOCHA 6 WANAOWEZA KUMRITHI TUCHEL BAYERN

**MUNICH,** UJERUMANI

MSIMU wa 2022/23 labda ulikuwa kiashirio cha kile kilichokuwa karibu na Bayern Munich.

Vikosi vya juu zaidi vya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, vimeshawishika kuachia kiwango chao katika kilele cha soka la Ujerumani.

Wakati wa miaka 11 kama timu bora ya ligi hiyo, hatimaye inaonekana kama Bayern watasalimisha taji lao la kudumu msimu huu.

Kocha Thomas Tuchel alisimamia ushindi mkubwa wa taji katika siku ya mwisho ya msimu uliopita na kuongezwa kwa Harry Kane kulikusudiwa kuongeza pengo kati ya Bayern na wengine. Hata hivyo, msimu wa 2023/24 umekuwa kampeni ya utendakazi duni pale 'Bavaria' na wiki ya jinamizi imemwacha Tuchel kwenye wakati mgumu.

Tishio linaloongezeka na ambalo sasa limeimarika kwa Bayer Leverkusen linaonekana kukaribia kuwaangusha wababe wa Bundesliga, huku kundi hili la wachezaji likitajwa kukumbukwa kama lile lililoruhusu koo la Bayern kwenye soka la Ujerumani kuteleza. Wakati huo huo, urithi wa Tuchel hautakuwa wa kupendeza.

Tayari Bayern imetangaza kuachana na kocha huyo mwishoni mwa msimu huu na uvumi kuhusu mrithi wake umeanza kuenea, na hapa 90min inawaangalia makocha sita wanaoweza kuchukua nafasi yake, twende sasa...

### #6. Ole Gunnar Solskjaer

Kocha wa zamani wa Manchester United, Solskjaer amekuwa akihusishwa na kazi hiyo kwa muda. Raia huyo wa Norway aliwahi kuinoa United baada ya kutimuliwa kwa Jose Mourinho mwishoni mwa 2018, na hatimaye kupata nafasi ya kudumu.

Solskjaer alifutwa kazi Old Trafford, lakini muda wake unaonekana kuwa wa kuvutia zaidi ukiangalia nyuma. Kikosi chake cha United kilikuwa na nguvu na uzembe, lakini aliweza kusawazisha kikosi na kukiongoza kwenye baadhi ya misimu iliyofanikiwa zaidi katika ulimwengu wa baada ya Sir Alex Ferguson.

Kama kocha, Solskjaer hakika linaweza kuwa si chaguo baya, lakini ni vigumu kumfikiria kuongoza meli pale Bayern - kutokana na ukosefu wake wa mahusiano na klabu hiyo kwa muda mrefu.

### #5. Antonio Conte

Harry Kane hakika atakaribisha ujio wa Conte kutokana na jinsi alivyofanya vema akiwa na Muitaliano huyo pale Tottenham Hotspur. Hata hivyo, wachezaji wengine wa kikosi cha Bayern huenda wasifurahishwe zaidi.

Bado, Conte ni kocha ambaye timu kama Bayern bila shaka zinaweza kumthamini kutokana na ustadi wake wa kimbinu na umakini wa kina.

Bayern wanaweza kufurahia mafanikio ya muda mfupi chini ya Mtaliano huyo katika mwaka wa kwanza. Itafurahisha kuona jinsi maadili ya Conte ya kiutendaji na ya Kiitaliano yanavyotafsiri kwenye nafasi ya Bundesliga.

Ushirikiano huu unaweza kufanya maajabu uwanjani, lakini uhusiano wa Conte na uongozi unaohusika sana wa Bayern bila shaka unaweza kuwa shida.

### #4. Hansi Flick

Bayern haipingani na muungano wa timu hiyo baada ya kumteua Jupp Heynckes mara 78, na kocha mkuu wa zamani wa Ujerumani, Flick anachukuliwa kuwa na uwezekano mkubwa kutua kwa Bavaria hao.

Flick aliingia katikati ya msimu wa 2019/20 kutokana na kuondoka kwa Niko Kovac na kuiongoza klabu hiyo kushinda mataji matatu ya kushangaza. Timu yake ya Bayern ilikuwa ya kuvutia sana; moja iliyobadilishwa na kanuni rahisi, lakini zenye ufanisi ambazo zilikuwa ishara ya klabu kubwa.

Timu hii ya Bayern haiko popote karibu kwa pamoja wala kuwa na kipaji kama msemo wa Flick wa kushinda kila kitu, lakini kocha huyo wa zamani ana ujuzi wa kubana kila kitu kutoka kwa kikosi hiki kinachopeperusha bendera.

Hata hivyo, taarifa za Barcelona kutaka kumnunua kocha huyo wa Ujerumani zinaweza kuwanyima Bayern kuungana naye tena.

### #3. Sebastian Hoeness

Wengine wanaweza kulia upendeleo ikiwa Hoeness atapata kazi, lakini kazi yake huko Stuttgart inamaanisha anazingatiwa na Bayern kwa sifa.

Mpwa wa mchezaji wa zamani wa Bayern na rais wa heshima Uli, Hoeness amefanya maajabu kule kusini-magharibi baada ya kuifundisha timu ya chini ya umri wa miaka 19 ya Bayern na timu ya akiba.

Miaka yake miwili akiwa Hoffenheim haikuwa ya kuridhisha, lakini ilijumuisha kichapo cha mabao 4-1 dhidi ya Bayern mnamo Septemba 2020. Akiwa Stuttgart, Hoeness amebadilisha timu kutoka ukingo wa kushuka daraja msimu uliopita na kuwa washiriki watarajiwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Akiwa na mbinu nyingi tofauti na miunganisho yake ya Bayern iliyoimarishwa, Hoeness ni mgombeaji wa chini wa wababe hao wa Ujerumani.

### #2. Zinedine Zidane

Zinedine Zidane kwenda Bayern ameanza kupata mvuto mwingi. Mfaransa huyo amekuwa hana kazi tangu aondoke Real Madrid kwa mara ya pili mwaka 2021.

Thomas Muller hivi majuzi alidokeza nia ya kuachana na kanuni kali za kucheza nafasi ambazo ziliabudiwa huko Munich wakati Pep Guardiola akiwepo. Naam, Zidane hakika atawezesha hilo.

Ingawa anavutia sana, Zidane si mvumbuzi wala si mchawi wa mbinu kama Nagelsmann na Tuchel. Kipaji chake kiko katika masuala ya usimamizi ambayo mara nyingi huenda chini ya rada yanapotathminiwa na watu wa nje.

Alikuwa na kikosi cha ajabu pale Madrid wakati wa ushindi wao wa mara tatu mfululizo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini haikuwa talanta pekee iliyoifanya 'Los Blancos' kuvuka mstari. Utulivu wa Zidane na uwezo wa kudhibiti ubinafsi uliiwezesha timu yake ya Madrid kufikia kilele ambacho hakijawahi kushuhudiwa.

### #1. Xabi Alonso

Hii itakuwa hatua kubwa zaidi kwa Bayern Munich. Kumzawadia mtaji bora zaidi wa usimamizi wa ligi - yule ambaye anaonekana kumaliza utawala wao wa miaka 11 kileleni - litakuwa jambo la kiwango cha juu zaidi.

Leverkusen ya Alonso ni nyota. Kipigo cha hivi majuzi cha kupigwa mabao 3-0 na Bayern kiliteka ukuu wao na ustadi wa mbinu wa Mhispania huyo. Alimzidi ujanja kabisa Tuchel, ambaye alikiri kuwa duni kwa kulinganisha na Leverkusen inayotumia mfumo wa 3-4-3 baada ya kutumia mfumo wa 4-2-3-1 kwa muda wote wa kampeni.

Kiungo huyo wa kati wa zamani wa Bayern anazingatiwa sana na Bavaria hao na inaonekana kuna pambano na Liverpool kwa huduma ya Alonso ambalo litaanza miezi ijayo.


Ingekuwa vema kwa Bundesliga kama Alonso angeepuka vuta nikuvute kutoka Bavaria, lakini huwezi kamwe kuweka dau dhidi ya Bayern katika hali kama hizi. Kawaida huishia na kile wanachotaka.

## Nukuu

"Nafikiri tu...kulikuwa na mjadala mkubwa kuhusu, 'je, Arsenal inahitaji nambari tisa?' Walichohitaji kufanya ni kuweka mpira wavuni. Trossard [Leandro] atafunga, Declan Rice amekuwa akifunga, Gabriel [Jesus] amekuwa akifunga, kwa hivyo haijalishi. Tukigeuza nafasi zetu kuwa mabao, tutakuwa - nadhani - timu ngumu sana kuifunga,**" Nguli wa zamani wa Arsenal, Thierry Henry.**



"Nawaheshimu sana mashabiki na Real Madrid, nikifunga sitashangilia, lakini nikibahatika kufunga na bao hilo linatosha kushinda, nitafurahi kwa sababu hizo pointi tatu zitanisaidia sana. Nitajisikia niko nyumbani kwa sababu nimekaa miaka mingi pale, nyakati muhimu zaidi za maisha yangu, nina kumbukumbu nzuri za mashabiki na wachezaji wenzangu. Itakuwa nyakati ya kipekee na ya kihisia,**" Beki wa Sevilla, Sergio Ramos, kabla ya jana kuivaa timu yake ya zamani, Real Madrid kwenye mechi ya LaLiga.**



"Nilikuwa na Arsenal kama mabingwa mwanzoni mwa msimu na si wengi walifanya hivyo, lakini bado nadhani City kwa wakati huu inaonekana kuwa mbaya. Lakini Arsenal, nataka Arsenal ifanye hivyo, kwa sababu za wazi, sitaki Liverpool kutwaa ubingwa,**" Beki wa zamani wa Manchester United, Gary Neville, hapendi kuona kikosi cha Jurgen Klopp kikitwaa ubingwa wa taji la Ligi Kuu msimu huu.**



# MAMBO 6 USIYOJUA SIMBA, YANGA CAF




Mfungaji wa bao la kwanza la Yanga dhidi ya CR Belouizdad Mudathir Yahya katika Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati wakishinda 4-0 juzi. MPIGAPICHA WETU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wawakilishi wengine wa Tanzania, Simba wanahitaji ushindi tu dhidi ya Jwaneng Galaxy kuweza kuingia hatua hiyo.

Juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ilifanikiwa kutinga hatua hiyo kwa kuibamiza CR Belouizdad kutoka Algeria mabao 4-0.

Kwa sasa inachosubiri ni kujua kama itashika nafasi ya kwanza au ya pili kwenye Kundi D, itakapocheza dhidi ya Al Ahly ya Misri katika mechi ya mwisho, itakayochezwa jijini Cairo, Machi Mosi, mwaka huu.

Ijumaa iliyopita, Simba nayo ilijiweka kwenye mazingira mazuri ilipolazimisha suluhu ugenini dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, katika Uwanja wa Felix Houphouet Boigny jijini Abidjan.

Simba inahitaji ushindi tu dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana ili kutinga kwenye hatua hiyo bila kutegemea matokeo ya mechi zingine.

Katika makala haya tumekusanya taarifa, takwimu, rekodi na mambo mengine ambayo yamekuwa na maswali mengi kwa timu za Tanzania kwenye uwakilishi wao msimu huu katika mechi hizo za kimataifa na hata Yanga ilivyotinga hatua ya robo fainali.

**1. Kanuni iliyowabeba Yanga robo**

Wengi wamekuwa na maswali na baadhi hawakuwa wanafahamu kuwa baada ya dakika 90 kumalizika Yanga ilikuwa imeshatinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa. Imewezekana na wengine bado hawajaelewa vema.

Kanuni ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (CAF), kwenye michuano hiyo inasema timu zinapolingana pointi basi itaangaliwa matokeo ya mechi zilipokutana zenyewe, maarufu kama 'head to head.'

Timu itakayokuwa na matokeo mazuri dhidi ya mwenzake ndiyo inayofuzu, na hii ni tofauti na kanuni ya kuangalia mabao ya kufunga na kufungwa kwa ujumla.

Yanga imefuzu baada ya kufikisha pointi nane ambazo hata kama zikifikiwa na CR Belouizdad ikicheza mechi ya mwisho dhidi ya Medeama hazitokuwa na maana yoyote, kwani nayo itafikisha pointi nane, lakini Yanga ilishinda mabao 4-0 nyumbani, Waalgeria wao walishinda 3-0, hivyo matokeo ya jumla kuwa 4-3.

**2. Kanuni hiyo pia itawabeba Simba**

Iwapo Simba itashinda mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy nayo itafuzu moja kwa moja robo fainali kwa kanuni hii hii iliyoipeleka Yanga robo fainali.

Simba ambayo itacheza mechi yake ya mwisho Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, iwapo itashinda itafikisha pointi tisa, ambapo hata kama Wydad Casablanca ikiifunga Asec Mimosas kwenye mechi ya mwisho itafikisha pointi tisa, kitakachowaamulia ni kile kile, timu hizo zilipokutana.

Simba ilipoteza bao 1-0 ugenini dhidi ya timu hiyo, lakini ikashinda mabao 2-0 nyumbani, hivyo itakuwa juu kwa jumla ya mabao 2-1.

**3. Yanga mabao manne kutoka nchi nne**

Mabao yote manne ya Yanga yaliyofungwa juzi yamepachikwa na wachezaji kutoka nchi nne tofauti.

Mtanzania, Mudathir Yahaya alianza kufungua njia, kabla ya Mburkina Faso, Stephane Aziz Ki kupachika la pili.

Raia wa Zambia, Kennedy Musonda, aliiwakilisha nchi yake kwenye kichapo dhidi ya CR Belouizdad, kabla ya Joseph Guede, kutoka Ivory Coast kugongelea msumari wa mwisho kwenye jeneza la Waalgeria hao.

**4. Robo fainali ya kwanza kwa Yanga**

Yanga inakwenda robo fainali kwa mara ya kwanza tangu mfumo wa Ligi ya Mabingwa Afrika uanzishwe.

Timu hiyo ambayo ilikuwa haijatinga kwenye hatua hiyo kwa miaka 25, imefanikiwa kutinga mara ya kwanza tangu 1998 na kwenda moja kwa moja hatua ya robo fainali.

**5. Simba pekee haijafungwa na Asec**

Rekodi kwenye Kundi B inaonyesha kuwa timu ya Simba ndiyo pekee ambayo haijapoteza mechi yoyote dhidi ya Asec Mimosas ambao ndiyo vinara na tayari wameshafuzu.

Suluhu ya juzi inahitimisha mechi mbili za sare kwa timu hizo mbili, kwani katika mechi ya kwanza zilitoka sare ya bao 1-1 Uwanja wa Benjamin Mkapa, kabla ya suluhu hiyo.

Asec Mimosas ikiwa nyumbani, iliifunga Wydad Casablanca bao 1-0 na ikiwa ugenini ikaitandika Jwaneng Galaxy mabao 2-0, kabla ya kuicharaza tena mabao 3-0 nyumbani.

**6. Simba yasaka robo fainali ya tano**

Wakati Yanga ikitinga robo fainali ya kwanza tangu kuanzishwa kwa mfumo huo, Simba inasaka robo fainali ya tano kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwani tayari imeshafanya hivyo mara nne.

Mara zote ilizokuwa ikitinga makundi kuanzia 2018/19, Simba imekuwa ikiishia hatua hiyo, ambapo mara zote ilifanikiwa kutinga robo fainali Ligi ya Mabingwa, ukiondoa msimu wa 2021/22 ambao ilicheza pia Kombe la Shirikisho barani Afrika.

**JE, WAJUA?**



MABAO mawili aliyofunga Harry Kane juzi wakati Bayern Munich ikishinda 2-1 dhidi ya RB Leipzig, yanamfanya kufikisha mabao 27 kwenye Bundesliga na 31 katika mashindano yote tangu ajiunge nayo akitokea Spurs msimu wa majira ya joto.





# Asasi za kiraia 11 zapewa kibali utoaji elimu mpigakura

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetoa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura kwa asasi za kiraia 11, katika uchaguzi mdogo wa udiwani kwenye kata 23 utakaofanyika Machi 20 mwaka huu.

Katika taarifa iliyotolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa NEC, ilieleza kuwa asasi hizo zimekidhi vigezo na kupewa vibali vya kutoa elimu hiyo.

Alizitaja asasi hizo kuwa ni Mbogwe Legal Aid Organization (MBOLAO) Isebya iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, Sustainable Hub for Policy Initiatives (SHPI) Mshikamano iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

Zingine ni Promotion and Women Development Association (PWDA) Kasingirima iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Bagamoyo Community Capacity Empowerment and Education (BCCEE) Fukayosi iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Action for Democratic Governance (A4DG) Kimbiji iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

Pia asasi ya Vanessa Foundation ambayo itatoa elimu katika Kata ya Nkokwa iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Tanzania Centre for Disability Development Initiatives (TCDDI) Nkokwa iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Safe Society Platform Tanzania (SSPT) Busegwe iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Butiama na Isebya iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe.

"Tumetoa kibali kwa Youth Against Aids and Poverty Association (YAAPA) ambayo itatoa elimu katika Kata ya Kasingirima iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Musoma Municipal Paralegal Organisation (MMPO) Mshikamano iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma."

"Shirika la Elimu ya Uraia na Uzalendo 'Civic Education and Patriotism Association' iliyoomba kutoa elimu katika kata za Kimbiji iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Msangani iliyopo katika Halmashauri ya Mji Kibaha, Fukayosi iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Mlanzi iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti na Kibata iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa," alisema.

Alizitaka asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura, kuzingatia Mwongozo wa Elimu ya Mpigakura wa Mwaka 2020 katika kipindi chote cha kutoa elimu hiyo katika uchaguzi mdogo.

Kadhalika, alisema NEC imetoa kibali kwa asasi za kiraia tatu ambazo zimekidhi vigezo kwa ajili ya kutazama uchaguzi huo.

Alisema asasi hizo ni Tanzania Alliance for Disability Development Initiatives itakayokuwa katika kata ya Mhande iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, Bridge Development Trust Organisation itakuwa katika Kata ya Buzilasoga iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema na Promotion and Women Development Association itayokuwa katika Kata ya Kasingirima iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (wa tatu kulia), akikata utepe ikiwa ishara ya uzinduzi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), jana mkoani Tabora, wa pili kulia ni Mkurugenzi wa benki hiyo, Frank Nyabundege na wa pili kushoto ni Mkuu wa Mkoa huo, Balozi Dk. Batilda Burian. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Serikali yakemea watoto kubebeshwa zigo la madaftari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, amewataka walimu wa madarasa ya awali kufundisha kwa kufuata mtaala na siyo kuwabebesha mzigo wa begi la madaftari watoto utakaowaletea athari za kiafya katika ukuaji wao.

Miaka mitatu iliyopita Nipashe ilichapisha makala kuhusu athari za ubebaji begi kubwa kwa wanafunzi, ambapo wataalamu wa afya walieleza athari watakazozipata ikiwamo kupinda mgongo.

Jana Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, akifungua mafunzo kwa walimu wa madarasa ya awali katika Mkoa wa Dodoma ambayo yamelenga kuwapa ujuzi wa kufundisha, alisema: "Kuna baadhi ya shule huko tunawabebesha watoto mzigo mkubwa kuliko umri wao, unakuta mtoto wa chekechea amebeba begi la madaftari 10 au 15 mpaka kibyongo, halafu anajazwa material (ujuzi) kibao unamfundisha mtoto wa awali hadi vitu vya darasa la saba."

Alisema walimu walioandaliwa vizuri na vinara wa elimu ya awali hawawezi kufanya hivyo na kuwataka kuzingatia mtaala na wasiwabebeshe mzigo wa begi watoto.

Aidha, alisema walimu hao wanapaswa kuwafundisha watoto kwa kuwalea kwasababu ndiyo kipindi ambacho wanakua ili kuwaandaa na kujiunga na elimu ya msingi.

Hivyo aliwahimiza walimu hao kuhakikisha wanawalinda watoto dhidi ya aina mbalimbali za ukatili kutokana na kukutana na kadhia wakati wa kwenda shule na kurudi nyumbani.

"Lakini ninyi kama walimu mna jukumu la kuwalinda watoto ili kuwakinga dhidi ya changamoto za ukatili zikiwamo za unyanyasaji wa kingono wanaofanyiwa majumbani, njiani wakati wa kwenda shule, shuleni kwenyewe ambapo kuna watumishi wasio waaminifu wamekuwa wakifanya vitendo vya ukatili kwa watoto," alisema Prof. Mdoe.

Alisema walimu hao wanapaswa kuwa marafiki wa watoto hao ili wawe wawazi kwao na kuwaeleza madhira wanayokumbana nayo hasa ya ukatili.

Kadhalika aliishukuru shirika lisilo la kiserikali linaloshughulia masula ya watoto wadogo (CiC) kwa namna linavyoshiriki katika uboreshaji wa elimu nchini.

Naye Mkurugenzi wa CiC, Craig Ferla, alisema shirika hilo linaamini mtoto akikua katika utimilifu wake Taifa nalo litakuwa.

# Hospitali zakumbushwa kuimarisha huduma kwa mteja

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imezielekeza hospitali, zahanati na vituo vya kutolea huduma za afya nchini kuimarisha huduma kwa mteja, kuunda mfumo wa dawati la kusikiliza maoni, kero na malalamiko ili kulinda haki za wagonjwa ikiwamo kutunza siri zao.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipofanya ziara ya kikazi kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa Dodoma, iliyolenga kukagua utendaji kazi na kuzungumza na watumishi wa hospitali hiyo.

Katika ziara hiyo aliambatana na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu na Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Best Magoma.

Alisema watoa huduma wanapaswa kuwa na weledi wenye kutumia lugha nzuri za staha pamoja na kulinda na kuzingatia haki za wagonjwa.

"Ni jukumu la kila mtumishi kuwahudumia wagonjwa sawa sawa kwa sababu tunategemea kila anayekuja kupata huduma ni mgonjwa, hivyo huenda akawa na hasira ila unatakiwa kumuhudumia na kumpokea vizuri na nilitoa maelekezo kwa hospitali zetu zote kuanzishwa kwa dawati la kusikiliza maoni, kero na malalamiko ya wateja ambalo linaonekana na kufikika na watoa huduma muda wote na wenye weledi na watakaokuwa na lugha za staha zinazozingatia mila na desturi zetu za kitanzania ikiwamo kutunza siri za wagonjwa," alisema.

Pia aliwahimiza watumishi katika sekta ya afya nchini kufanya kazi kama timu na kudumisha ushirikiano ili kuzidi kuimarisha na kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma bora kwa Watanzania.

Dk. Jingu alipongeza watumishi wa hospitali hiyo kwa ubunifu wa utoaji wa huduma bora na nzuri wagonjwa, usafi wa mazingira ya hospitali na ushirikiano walioutoa wakati wa janga la maporomoko ya Wilaya ya Hanang.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Tumaini Nagu, alipongeza kwa huduma bora zinazotolewa na watumishi wa hospitali hiyo hasa katika huduma za uzazi.

Hivyo aliwataka watumishi kuzidi kuongeza umakini na kuwapo kwa miongozo na taratibu ya utekelezaji wa majukumu yao katika vitengo vyote vya kutolea huduma ili kupunguza makosa ya kitabibu.



# Waomba sukari kutoka Malawi, Zambia kuingizwa nchini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wameiomba serikali kuruhusu sukari kutoka nchi za Malawi na Zambia kuingizwa nchini bila masharti ya kiforodha ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa bidhaa hiyo na kupunguza bei.

Wamesema bei ya sukari kutoka kwenye mataifa hayo inauzwa kwa bei ndogo kuliko ya Tanzania, lakini wakitaka kuinunua wanakutana na vikwazo vya kiforodha ambavyo wakivitekeleza bado bei inakuwa juu.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki, baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya walisema bidhaa hiyo imeadimika na hata inayopatikana ni kidogo, inauzwa kwa bei ya juu ambayo wanashindwa kuimudu.

Mmoja wa wananchi hao, Mariam Mwakibasi mkazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ambaye pia ni mama lishe alisema awali walikuwa wananunua sukari kwa Sh. 2,500 na 2,800 lakini kwa sasa wananunua kwa Sh. 4,500 na 5,000 bei ambayo alisema haijawahi kupanda kwa kiwango hicho. Alisema kutokana na kupanda kwa bei hiyo hata wao wamelazimika kupandisha bei ya bidhaa zinazotokana na sukari ikiwemo mandazi, chapati na chai, hali ambayo imesababisha kuanza kukosa wateja.

Alisema kwa sasa sukari ya kutoka Malawi na Zambia imeanza kuingia kwa njia za magendo, lakini bado haziwasaidii kutokana na waingizaji kuuza kwa bei inayokaribiana na ya Tanzania.

"Maandazi ambayo tulikuwa tunauza Sh.200 sasa hivi tunauza Sh. 300, chapati tulikuwa tunauza mbili kwa Sh. 500 sasa hivi chapati moja tunauza Sh. 300 na wengine wanauza Sh. 400 mpaka Sh.500, sasa ni kitu ambacho wateja wetu hawajazoea na hivyo wameanza kutukimbia," alisema Mariam.

Jailos Kijalo alisema sukari kutoka Malawi na Zambia zinauzwa maeneo ya mipakani kwa kati ya Sh. 2,500 na 2,700 lakini haziruhusiwi kuingizwa nchini bila kulipiwa ushuru hali ambayo inasababisha bei ya bidhaa hiyo kuendelea kuwaumiza wananchi.

Alisema anafanya biashara zake kati ya Mji wa Tunduma, Jiji la Mbeya na Kyela lakini amekuwa akishuhudia maofisa wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) wakiwakamata wananchi wanaosafirisha sukari ya Malawi na Zambia kupeleka Mbeya.

Alisema maofisa hao huwa wanaingia kwenye magari ya abiria na kukagua na kwamba wakiikuta sukari hiyo wanataifisha na wakati mwingine wanamchukulia hatua mwenye gari.

"Sasa hivi sukari za Zambia na Malawi zinauzwa kama bangi, wafanyabiashara wanauza kwa kificho japo ndiyo inasaidia watu, sukari yetu haipatikani kabisa na hata ukiipata unaunua kwa bei ya juu sana, kwahiyo binafsi nashauri serikali ilegeze masharti ya uingizaji wa bidhaa hii kutoka nchi hizi jirani," alisema Kijalo.

Mmoja wa wafanyabiashara wa Jiji la Mbeya ambaye hakutaka jina lake litajwe alisema kwa sasa sukari ya Tanzania inauzwa kwa bei ya kati ya Sh.95,000 na Sh.100,000 kwa katoni yenye uzito wa kilogramu 20 na kwamba pamoja na bei hiyo bado haipatikani. Alisema wafanyabiashara wakubwa wanauza bidhaa hiyo kwa kificho na kwamba kama hawajakuzoea hawauzi hali ambayo inasababisha bidhaa hiyo kuendelea kuadimika. "Hata mimi nikiipata kwa bei hizo nalazimika kuuza Sh.5,000 ili angalau nisiwapoteze wateja wangu, kwa sasa sukari kwangu siyo biashara kwa sababu sipati faida yoyote na wakati mwingine huwa naona bora nisiwe nayo ili kuepuka sheria kwa sababu tunawindwa," alisema mfanyabiashara.



Mmoja wa wakulima wa viazi mviringo wa Kijiji cha Kikondo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, akipakia viazi kwenye mfuko mwishoni mwa wiki baada ya kuvuna tayari kwa kuuza. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanaume msiwape 'stress' wake zenu wanaonyonyesha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAUME wametakiwa kuwapatia ushirikiano wenza wao wanaonyonyesha ili kuwaepuka kupata msongo wa mawazo ambao utawasababisha upungufu wa maziwa wakati wa kunyonyesha.

Wito huo umetolewa na Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Itika Mlagila wakati wa kongamano la kuhitimisha mafunzo ya malezi na makuzi kupitia mtandao yaliyoandaliwa na Shirika la WeCare Foundation yenye kaulimbiu isemayo 'Elimika sasa kwa njia ya mtandao'.

Mafunzo hayo yalikuwa yanatolewa kwa familia zenye kinamama wajawazito na wenye watoto wachanga kwa lengo la kuwaandaa kunyonyesha vizuri watoto wao.

Alisema hakuna mama mwenye maziwa machache kama ambavyo baadhi ya wananchi wamekuwa wakidhani na kwamba zipo sababu ambazo husababisha tatizo hilo na moja ya sababu ni msongo wa mawazo.

Alisema ufumbuzi mojawapo kwenye kupambana na tatizo hilo ni kuwa karibu na mwenza kipindi cha unyonyeshaji na siyo kuwakimbia kama ambavyo baadhi wamekuwa wakifanya.

Vilevile alisema kundi hilo linaweza kupata tatizo hilo kutokana na kunyanyaswa ama kufanyiwa ukatili wa kijinsia ambao utasababisha kuwa na msongo wa mawazo.

"Wengi wetu tumezoea kulalamika 'ooh mimi sina maziwa mengi!' hapana hakuna mama aliye na maziwa mepesi wala machache, zipo sababu zinazoleta hali hiyo na miongoni mwa hizo ni mama kuwa na 'stress' (msongo wa mawazo), alisema Mlagila.

Vilevile alisema wanawake wavivu wa kunyonyesha huwa wanasingizia kuwa hawana maziwa ya kutosha ama wana maziwa mepesi jambo ambalo alisema siyo kweli.

Mratibu Msaidizi wa Chanjo wa Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya (MZRH) Kitengo cha Wazazi Meta, Zena Sambala aliwataka kina mama wajawazito na wanaonyonyesha kuhudhuria kliniki au matibabu mengine kwenye vituo vya kutoalea huduma za afya wakiwa wameambatana na wenza wao.

Alisema utaratibu huo unasaidia wenza hao kupata uelimu ya pamoja kuhusu mambo muhimu yanayohitajika kufanyika kwa ajili ya maendeleo ya ujauzito na makuzi ya watoto.

Sambala alisisitiza watoto wanaopata matatizo baada ya kupatiwa chanjo kurejeshwa kwenye vituo walivyopewa huduma ili wafanyiwe uchunguzi.

Mmoja wa wanufaika wa elimu hiyo kupitia kundi songozi la Whatsapp alisema yeye alianza kupata elimu tangu alipopata ujauzito mpaka sasa na kwamba elimu hiyo imemsaidia kumlea mtoto wake vizuri kwa kuzingatia kanuni ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (MMMAM).

Mkurugenzi Mtendaji wa WeCare Foundation, Elizabeth Maginga, alisema waliamua kuanzisha mafunzo ya MMMAM kupitia mtandao ili kuwafikia kwa urahisi wahitaji wa elimu hiyo.

## Mbunge 'awafuta machozi' wanafunzi Shule ya Mpuguso

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Mpuguso wilayani Rungwe mkoani Mbeya, wanalazimika kukaa kwa kusongamana darasani kutokana na tatizo la upungufu wa madawati.

Kutokana na tatizo hilo Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo amekabidhi madawati 30 ili kupunguza tatizo hilo.

Akizungumza wakati akikabidhi msaada huo, Fyandomo aliwataka wadau mbalimbali wa maendeleo kusaidia maeneo yenye matatizo kwenye sekta ya elimu ili kuiunga mkono serikali kutokana na maendeleo ambayo inayafanya.

Fyandomo alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali katika kuimarisha sekta ya elimu nchini, wadau mbalimbali wana nafasi ya kuunga mkono jitihada hizo kwa kutatua kero mbalimbali ikiwemo upungufu wa madawati.

"Serikali imeweka elimu bila malipo ili kuhakikisha watoto wetu wote wanapata haki yao ya kielimu na kutimiza ndoto zao, hivyo ni muhimu na sisi tukachangia kutatua hizi kero ambazo ziko ndani ya uwezo," alisema Fyandomo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Thomas Mwanga, alisema halmashauri hiyo ina mikakati ya kushirikisha wadau mbalimbali katika kuhakikisha tatizo la upungufu wa madawati linaisha.

Alimshukuru mbunge huyo kwa kuchangia madawati hayo na kuwataka viongozi wa shule hiyo kuhakikisha madawati hayo yanatunzwa vizuri ili yaweze kutumika kwa muda mrefu.

Diwani wa Kata ya Mpuguso, Japhet Mwakagugu, alisema madawati yaliyotolewa yamewapunguzia mzigo wa upungufu uliokuwepo na kuwataka wananchi wa kata hiyo kuwaunga mkono viongozi na wadau mbalimbali wanaojitoa kuchangia maendeleo.



# Walimu madrasa watakiwa kutumia elimu kuboresha maadili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haruna Ali Suleiman, amewataka walimu wa madrasa kuitumia vyema elimu waliopatiwa ili kuboresha maadili ya watoto na kupata taifa bora.

Akizungumza jana wakati akifunga mafunzo ya walimu wa madrasa kwa Wilaya ya Kusini, katika Shule ya Ufundi Kiongoni Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja, alisema endapo mafunzo hayo yatatumika ipasavyo yataenda kubadilisha maisha ya wanafunzi hao.

Aidha, aliitaka ofisi ya mufti kuyaendeleza mafunzo hayo hadi kufikia ngazi mbalimbali ili wanafunzi wa madrasa wapate elimu bora inayoendana na wakati.

Hata hivyo alisema kuwa kutokana na masomo waliyopatiwa walimu hao yatawasaidia kupata ujuzi na kujua njia bora za kujifunza na kufundishia, pamoja na kubadilisha dhana ya ufundishaji madrasa.

Naye Katibu Mtendaji Ofisi ya Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, aliwataka walimu wa madrasa kuwasimamia vyema wanafunzi na kuondoa mianya yote inayopelekea kutokea kwa vitendo vya udhalilishaji.

Alisema endapo madrasa hazitakuwa na uwiano wa walimu wa kike na wakiume na kuwakusanya wanafunzi nyakati za usiku vitendo vya udhalilishaji vinaweza kutokezea.

Aidha, aliwaomba walimu wa kiume kuacha kukaa faragha na wanafunzi wa jinsia moja au tofauti na ni miongoni mwa vichocheo vya vitendo hivyo.

Hata hivyo alisema mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo walimu wa madrasa juu ya mbinu mpya za kufundishia wanafunzi wa madrasa ili kuinua ufahamu wao.

Walimu hao waliahidi kuyafanyia kazi ipasavyo mafunzo hayo pamoja na kuzitumia mbinu mbalimbali walizopatiwa ili kuimarisha elimu ya madrasa kwa wanafunzi.

# Mfumo wa kidigitali Zan Vibali kuanza wiki hii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUNGEZI Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao, Said Seif Said, amesema mfumo wa kidigitali wa Zan Vibali utaanza kutumika Machi mwaka huu.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya mfumo huo yaliyoshirikisha wakuu wa taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Said alisema lengo la kuwa na mfumo huo ni kurahisisha utaratibu wa uombaji wa vibali na mfumo huo unamwezesha mtu popote alipo kupeleka maombi yake na kufika kwa mlengwa.

"Hata saa sita za usiku ukiwa upo kwako unaweza kuleta maombi yako yakafika kwa mlengwa na yeye akaweza kutia mchango wake na ikafika mpaka kwa Katibu Mkuu Kiongozi naye akatoa kibali, hivyo mfumo huu umerahisisha utaratibu mzima na kuleta ufanisi katika uombaji wa vibali," alisema.

Alisema kuwa ni azma ya serikali ya kuleta mabadiliko na kutumika kwa mfumo huo ili kuleta uwazi katika maombi ya vibali na hata wale wanaosafiri kwenda nje ya nchi watarahisishiwa.

Said alisema kabla ya mfumo huo utaratibu uliokuwa ukitumika kwa kuandika maombi kwa kutumia makaratasi mfumo ambao kwa sasa umepitwa na wakati.

Hivyo, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo wanapopata changamoto katika kutumia mfumo huo wasisite kuuliza, kwamba Wakala Mtandao Serikali umejipanga kutoa ushirikiano kwa taasisi yoyote ambayo itapata changamoto katika utumiaji wa mfumo huo.

Pia aliahidi E-Government itatoa mafunzo hayo kwa upande wa Pemba ili kuhakikisha watumishi wote wa serikali wanapata mafunzo ya kutosha na wote wanakuwa nafasi moja katika utumiaji wa mifumo inayoanzishwa na serikali.

Naye Mkurugenzi wa Utawala Wakala wa Serikali Mtandao, Khamis Mtumwa Ali, alisema mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwapa uelewa maofisa TEHAMA na maofisa utumishi, kufahamu jinsi gani ya kutumia mfumo wa Zanvibali.

Alisema mfumo huo ni mwarobaini wa kuhakikisha vibali vya kwenda nje vinapatikana kwa wakati na changamoto ambazo mwanzo zilikuwa zikijitokeza zinatatuliwa kwa kiasi kikubwa kupitia mfumo huo.

Alisema mkakati mkubwa wa serikali inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kuhakikisha Zanzibar inakwenda kidijitali.

Alisema zipo nchi ambazo zinapiga hatua kubwa za kimaendeleo, hivyo wakala imehakikisha takwa hilo la Rais linafikiwa kutoka katika mifumo ya zamani ya kutumia karatasi na kuingia katika mifumo ya kimtandao ili kurahisisha utoaji wa huduma.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa na yanamwezesha mfanyakazi kuomba ruhusa kwa kutumia mfumo na kuondosha kuomba kwa kutumia makaratasi.

Othman Ali Abass kutoka Wakala wa Majengo na Asha Hija Ofisa Utumishi Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali walisema hatua hiyo inarahisisha kupunguza mlolongo mrefu katika kuomba kibali.




Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja na Kidigiti wa Vodacom Tanzania, Belinda Wera (kushoto), akiwa na Meneja Makusanyo, Charles Daniel, wakiwa wameshikilia vyeti walivyokabidhiwa baada ya kushinda tuzo tatu za huduma bora kwa wateja kwa mwaka 2023 zilizoandaliwa na Chartered Institute of Customer Management (CICM) mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Kampuni hiyo ilishinda vipengele vya utoaji huduma bora kwa wateja (mshindi), mtandao bora wa huduma za mawasiliano na intaneti (mshindi wa pili) na uwajibikaji kwa shughuli za kijamii (mshindi wa pili). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Idadi ya watalii wanaoingia Zanzibar yazidi kupaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDADI ya watalii 73,468 waameingia nchini katika kipindi cha Januari 2024, likiwa ni ongezeko kubwa kulinganisha na kipindi cha Desemba mwaka jana ambapo waliingia watalii 70,186.

Mtakwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Khamis Abrahman Msham, alitoa taarifa hiyo juzi wakati akiwasilisha takwimu za uingiaji wageni kwa kipindi cha Januari mwaka huu.

Msham alisema nchi ya Poland iliongoza kuleta watalii zaidi ikifuatiwa na Ufaransa. Alisema kati ya idadi hiyo watalii 59,635 walioingia nchini walitoka Ulaya, 5,922 walitoa nchi mbalimbali za Afrika.

Hata hivyo aliwasisitiza wadau wa sekta ya utalii kuimarisha zaidi huduma katika sekta hiyo ili nchi iweze kupokea wageni wengi na utalii uweze kukua sambamba na kuongeza pato la taifa.

Naye Ofisa Utafiti na Takwimu kutoka Kamisheni ya Utalii, Maabadi Jafar Muhidini, alisema sababu zilizochangia kuongezeka kwa idadi hiyo ni pamoja na kuwasili wa meli kubwa nchini kwa ajili ya kuona maeneo ya vivutio vya kitali.

"Kwa kipindi hiki tumeshuhudia kuingia kwa meli kubwa za kitalii ambazo zilikuwa na idadi kubwa ya watalii waliokuja kutembelea Zanzibar na kuona vivutio mbalimbali vilivyopo nchini", alisema.

Mrakibu Msaidizi kutoka Idara ya Uhamiaji, Rashid Abdallah Ali, alisema watahakikisha wnaendelea kutoa huduma bora na usalama kwa wageni hasa wanaotumia mipaka ya baharini.

Alisema pia wamejipanga katika eneo hilo kuhakikisha kunakuwa na usalama kwa wageni wanaoingia na kutoka.

Ofisa kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Paul Lawuo, alisema sekta ya utalii ina umuhimu mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi na kuimarisha pato kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

# Mbaroni tuhuma kukutwa na vipande vya meno ya tembo

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

EDSON Mahmoud (44), mkazi wa Tarafa ya Nyamiaga, wilayani Ngara, mkoani Kagera anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kukutwa na vipande vitatu vya meno ya tembo kinyume cha sheria.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Blasius Chatanda alisema jana kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa Februari 21, mwaka huu saa nne asubuhi katika kata ya Benaco, wilayani humo.

Alisema kuwa askari wake walikamata mtuhumiwa huyo akiwa na meno hayo wakati anayasafirisha kwa pikipiki yenye namba za usajili MC 977 DGZ kwenda kuuza.

Alisema mtuhumiwa alikuwa na wenzake watatu ambao walitoroka baada ya kusikia mwenzao amekamatwa.

Kamanda huyo alisema kuwa baada ya kukamata meno hayo, yalipimwa na kubainika kuwa na uzito wa jumla ya kilo 12. Sasa msako unaendelea ii kubaini wote wanaojihusisha na biashara hizo haramu.

"Jeshi linatoa onyo kwa vitendo haramu vinavyoendekezwa ili kujipatia kipato kwa njia zisizo halali na zenye madhara kwa jamii. Niseme tu wanaofanya hivyo watafute shughuli halali ya kuwaingizia kipato," alionya kamanda huyo.

Aliomba wananchi kuendelea kushirikiana na jeshi hilo kuhakikisha wanatoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili kuongeza udhibiti wake.

Kuhusu mtuhumiwa huyo, Kamanda Chatanda alisema uchunguzi unaendelea ili kubaini chanzo na wahusika wengine na ukikamilika, atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, akisalimiana na Makamu Rais Mwandamizi - Kitengo cha Masuala ya Ubia/Ushirika Afrika kutoka AngloGold Ashanti - GGML, Terry Strong na Meneja Mwandamizi wa Masuala ya Rasilimali Watu kutoka GGML, Charles Masubi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Shigela: Nidhamu ndiyo nguzo ya mafanikio kazini

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, amewataka wahitimu wa vyuo vikuu waliojiunga na programu ya mafunzo tarajali katika Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kufanya kazi kwa bidii, kuwa wabunifu na nidhamu.

Pia amewataka wahitimu hao kutumia fursa zinazopatikana ndani na nje ya mgodi huo ili kujiendeleza na kuondoka wakiwa tofauti na namna walivyoingia kwenye programu hiyo ya mwaka mmoja. Shigela alitoa rai hiyo wiki iliyopita mjini Geita wakati wa hafla ya kukaribisha wahitimu 40 wa vyuo vikuu ambao wamejiunga na GGML kwa mwaka 2024/25 kupata mafunzo tarajali sambamba na wahitimu wengine 10 wa programu hiyo kwa mwaka jana ambao wameendelea na mafunzo ya juu zaidi baada ya kupata ajira ya kudumu ndani ya GGML.

Wanafunzi hao 10 waliomaliza programu mwaka jana, wamechaguliwa kuendelea na programu mpya inayofahamika kwa jina la African Business Unit Graduate (ABU) ambayo inawapa fursa ya kubadilishana uzoefu na wahitimu wa aina hiyo katika nchi nyingine za Ghana na Guinea ambako AngloGold Ashanti, kampuni mama ya GGML inamiliki migodi.

Shigela alisema nidhamu kwa wahitimu hao ni msingi muhimu katika utumishi wa aina yoyote, hivyo wanapaswa kuzingatia nidhamu katika utendaji wao na hata wanapokengeuka kutekeleza majukumu yao nafsi inapaswa kuwasuta.

Alitoa mfano kuwa wapo wanafunzi ambao walikwenda kupata mafunzo tarajali ndani ya kampuni hiyo na kufanikiwa kupata leseni za uchimbaji kwa ngazi mbalimbali nje ya mgodi na sasa ni matajiri.

Pia alisema kwa kuwa mzunguko wa ununuzi wa ndani ya GGML unakaribia Sh. trilioni moja kwa mwaka hasa ikizingatiwa kampuni hiyo inazingatia matakwa ya sheria ya 'Local content' ambayo inaitaka kufanya ununuzi wa bidhaa zake nchini, nayo ni fursa nzuri kwa wahitimu hao kujifunza na kufungua kampuni za kusambaza bidhaa kwa mgodi huo.

Mbali na kuipongeza GGML kwa kuwa na mipango madhubuti inayofungua fursa kwa vijana wa kitanzania, pia alipongeza wahitimu hao ambao wamefanikiwa kupenya na kupata nafasi hiyo hasa ikizingatiwa walioomba nafasi hiyo walikuwa 2,800, lakini wamechaguliwa 40 pekee.

Meneja Mwandamizi anayeshughulikia masuala ya rasilimali watu, Charles Masubi alisema programu hiyo ya ABU ambayo inahusu wahitimu 10 wa mwaka jana, itawawezesha kupata mafunzo ya juu zaidi ya ujuzi wao wa darasani.

"Kama ni mhandisi tutamfundisha namna ya kuingia makubaliano, kuandaa bajeti, lakini kupata ujuzi wa namna ya kuwasiliana kwa usahihi na wenzake," alisema.

Alisema lengo la programu hiyo ni kuwaandaa wafanyakazi wabobezi ambao wanaweza kuja kuwa viongozi wa baadaye wa kampuni hiyo na hata nje ya GGML.

Mmoja wa wahitimu aliyepata fursa ya mafunzo tarajali kwa mwaka huu, Fakii Juma alisema GGML ina matarajio makubwa kwao katika uzalishaji, hivyo watatumia vipaji vyao kuongeza ujuzi kwenye mgodi huo kutokana na elimu wanayoipata na wanajivunia kwamba wataongeza thamani ya mgodi huo.

# Tanzania na Burundi kuimarisha mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA na Burundi zimeingia makubaliano ya kibiashara kati ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Taasisi ya Burundi Backnone System (BBS) kuongeza ufanisi wa huduma kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mkataba huo wa miaka mitano wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 3.3 (Sh. bilioni 8.3), ulitiwa saini mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam na kushuhudiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Peter Ulanga, alisema Burundi kupitia BBS, imeamua kuongeza mahitaji ya huduma za mkongo wa mawasiliano kutoka Tanzania kutokana na mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa ushirikiano wa kiteknolojia baina ya Tanzania na Burundi mwaka 2019.

"Tunajivunia uhusiano wetu tangu mwaka 2019. Baada ya matokeo mazuri ya huduma za Mkongo wa Taifa, jirani zetu Serikali ya Burundi kupitia Burundi Backbone System wamekubali kuongeza huduma kutoka kwenye Mkongo wa Taifa wa mawasiliano, kwa mkataba wa kibiashara wa miaka mitano," alibainisha Ulanga.

Kwa kutambua mchango wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mtendaji Mkuu wa BBS, Jeremie Diomede Hageringwe, baada ya utiaji saini mkataba wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, alimkabidhi zawadi Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, ambaye aliahidi kuendeleza ushirikiano wa kitaalamu baina ya mamlaka hizo za usimamizi wa mawasiliano.

TCRA inaendelea kuwa mshirika muhimu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Burundi.

Tanzania ni mshirika muhimu katika usambazaji wa huduma za mkongo wa mawasiliano kwa nchi za Afrika Mashariki na Burundi ni miongoni mwa nchi zinazonufaika na ushirikiano huo wa kiteknolojia kwa kuunganishwa na Mkongo wa Mawasiliano kutoka Tanzania.

Nchi zingine zinazonufaika ni Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Malawi na Msumbiji.

## HABARI KIMATAIFA

# ECOWAS yakubali kuondoa vikwazo vyake kwa Niger

**Abuja,** NIGERIA

JUMUIYA ya Kanda ya Afrika Magharibi (ECOWAS), imetangaza kuondolewa kwa vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Niger.

Hayo yalifikiwa katika mkutano wa viongozi mjini Abuja, wakitaka kupitisha mkakati mpya wa kuzishawishi nchi zinazoongozwa na wanajeshi kusalia katika umoja huo.

Vikwazo vya awali vililenga shughuli za usafiri, biashara na uchumi nchini kwa lengo la kupinga mapinduzi ya Julai 26, mwaka jana na baadhi ya maofisa wa kijeshi.

Rais wa Tume ya ECOWAS, Omar Alieu Touray ambaye alisoma maamuzi yaliyofikiwa na viongozi wa ECOWAS, alisema kuwa kuondolewa kwa vikwazo dhidi ya Niger ni "kwa misingi ya kibinadamu" ili kupunguza mateso yaliyosababishwa na matokeo yake.

Viongozi wa kijeshi wa majirani watatu wa Sahel pamoja na Guinea sasa wako huru kushiriki katika masuala ya kiufundi na usalama ya umoja huo.

ECOWAS pia imetoa wito wa kuachiwa huru kwa rais aliyeondolewa madarakani Mohamed Bazoum, na kuzitaka nchi hizo nne kuwasilisha ratiba zao za mpito wa kidemokrasia.
**BBC**




Rais wa Nigeria ambaye ni Mwenyekiti wa ECOWAS, Bola Tinubu. **PICHA: MTANDAO**

# Waandamana wakiisubiri tarehe uchaguzi Senegal

**Dakar,** SENEGAL

MAMIA ya raia wa Senegal waliandamana katika mji mkuu wa Dakar, kumuunga mkono na wengine wakimpinga Rais Macky Sall.

Maandamano hayo yamefanyika wakati taifa hilo likiwa katikati ya mgogoro wa kisiasa uliotokana na kucheleweshwa uchaguzi wa rais uliokuwa umepangwa kufanyika, jana, Jumapili.

Maandamano ya kumpinga rais yametokana na wito uliotolewa na muungano wa vyama vya kisiasa na asasi za kiraia, F24, unaotaka uchaguzi ufanyike.

Nao waandamanaji wanaomuunga mkono Rais Sall walikusanyika katika eneo la makazi ya watu mjini Dakar, wakiwa wamebeba bendera za Senegal wakitetea rekodi yake na kusema kuwa amefanya mengi. Rais huyo wa Senegal amekumbana na upinzani mkali tangu alipotangaza kuchelewesha uchaguzi wa rais wa Februari 25.

Hata hivyo Baraza la Katiba la nchi hiyo, liliupindua uamuzi huo na kutaka uchaguzi uitishwe haraka iwezekanavyo. **DW**

# G7 yataka ufafanuzi kifo cha Navalny

**Roma,** ITALIA

KUNDI la mataifa saba yaliyostawi zaidi kiviwanda duniani (G7), limeitaka Russia, kufafanua kikamilifu mazingira ya kifo cha kiongozi wa upinzani nchini humo, Alexei Navalny.

Navalny, alijitolea maisha yake kupigana dhidi ya Kremlin na ikiwamo uchaguzi huru na wa haki.

Baada ya majuma mawili ya mvutano na mamlaka ya Russia, hatimaye mamake Alexeï Navalny, amepokea mwili wa mwanawe.

Tangazo hilo lilitolewa kwenye mitandao na timu ya wapinzani, ambayo ilifafanua kuwa bado haijajua ni wapi na chini ya mazingira gani mazishi ya Navalny, yatafanyika.

Msemaji wa kiongozi huyo wa upinzani, Lyoudmila Navalnaïa, bado yuko Salekhard kuchukua mwili wa mtoto wake.

Kira Yarmish, alifafanua kwamba bado hajui ikiwa viongozi watazuia mazishi kufanyika kama familia inavyotaka na kama Alexei Navalny, anastahili.

Siku mbili zilizopita, mama mzazi wa Navalny, Lyoudmila Navalnaïa, alirusha video mitandaoni akiishutumu mamlaka.

Alibaini kwamba walitaka kumkabidhi mwili wake kwa sharti tu kwamba mazishi ya mwanawe yafanyike kwa siri.

Bado hakuna habari iliyovuja juu ya uwezekano wa makubaliano kati ya mamlaka na mama wa kiongozi huyo wa upinzani.

Mara moja, timu nzima ya Alexeï Navalny, ambayo inaishi uhamishoni nje ya Russia, imewashukuru kwenye mitandao makumi ya maelfu ya watu ambao walimtolea wito hadharani Vladimir Putin, ili mwili wa Navalny ukabidhiwe familia yake.
**RFI**

## Lukashenko atangaza kuwania urais 2025

**Minsk,** BELARUS

KIONGOZI wa Belarus, Alexander Lukashenko, amesema anagombea tena urais katika uchaguzi mwaka 2025.

Tangazo hilo limetolewa mwishoni mwa wiki na shirika la habari la Belarus BelTA.

Lukashenko, alitoa tamko hilo mbele ya waandishi wa habari, baada ya kushiriki kupiga kura za bunge na serikali za mitaa.

Akiendelea kujibu maswali ya waandishi wa habari alisema, atatetea kiti chake kwa kuwa hakuna mtu, wala rais muwajibikaji anayeweza kuwaacha raia wake waliomuunga mkono wakati wa mapambano.

Rais huyo mwenye miaka 69, ameitawala Belarus tangu mwaka 1994 na ni mmoja wa washirika wa karibu wa Rais wa Russia, Vladimir Putin.

Hata hivyo alisema, mwaka mmoja hadi kufanyika kwa uchaguzi wa huo wa rais ni kipindi kirefu na mambo mengi yanaweza kubadilika.
**DW**

## Marekani, Uingereza zawashambulia Wahouthi

**Washington,** MAREKANI

VIKOSI vya Marekani na Uingereza, vimefanya mashambulizi mapya dhidi ya maeneo 18 ya waasi wa Kihouthi nchini Yemen.

Marekani na Uingereza zimesema mashambulizi yalilenga hasa maghala ya silaha na ndege zisizo na rubani.

Vikosi hivyo, vimefanya mashambulizi mapya dhidi ya maeneo 18 ya waasi wa Kihouthi nchini Yemen.

Hayo yanajiri ikiwa ni wiki kadhaa baada ya mashambulizi dhidi ya meli zinazosafirisha mizigo katika Bahari ya Shamu, yaliyofanywa na waasi hao wanaoungwa mkono na Iran.

Katika kauli ya pamoja, Marekani na Uingereza zilisema mashambulizi yalilenga hasa maghala ya silaha, ndege zisizo na rubani zinazotumiwa kushambulia, mifumo ya ulinzi wa anga, rada na helikopta.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, alisema nchi yake haitasita kuchukua hatua kuyalinda maisha na uhuru wa kibiashara katika moja ya njia muhimu za usafirishaji mizigo duniani.

Lakini kundi hilo la Wahouthi nalo limeapa kuwa litapambana na mashambulizi hayo ya Marekani na Uingereza. **VOA**

# TWIGA STARS AKILI WAFCON IKIIVAA BANYANA BANYANA

Na Saada Akida

WAKATI Twiga Stars ikiwa na kibarua kigumu cha kupindua meza nchini Afrika Kusini dhidi ya Banyana Banyana, katika mechi ya kuwania kufuzu Olimpiki, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, amesema mechi hizo mbili zitamsaidia kujenga kikosi imara kujiandaa na Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON) 2024, zitakazofanyika nchini Morocco.

Kauli ya kocha huyo inakuja baada ya kupoteza mechi ya kwanza nyumbani dhidi Banyana Banyana kwa kukubali kichapo cha mabao 3-0, hivyo kuelekea mchezo wao wa marudiano kesho watakitakiwa kushinda kuanzia 4-0 ili kusonga mbele.

Tayari kikosi cha Twiga Stars kimewasili salama nchini Afrika Kusini chini ya kocha wake, Shime ambaye alisema licha ya kupoteza mechi ya kwanza nyumbani, bado ana matumaini makubwa na vijana wake kufanya vizuri.

**Alisema mechi ya kwanza walizidiwa kwa ubora wa mchezaji mmoja mmoja, lakini wamejifunza kitu kutoka katika mchezo huo hasa kuelekea kwenye maandalizi yao ya fainali za WAFCON.**

"Tukumbuke tunacheza na timu kubwa, tunezidiwa mechi ya kwanza, lakini tumejifunza kwa sababu hii timu inayoshiriki michuano ya kufuzu Olimpiki ndio itakayowakilisha Tanzania katika WAFCON, tutatumia kama mafunzo ili kutusaidia mbele.

"Kwa sasa tunaendelea kusahihisha makosa yetu na kujiandaa kwa mechi ya marudiano dhidi ya Afrika Kusini, ninaimani tutapambana kupata matokeo ugenini kama wao walivyotufunga nyumbani," alisema kocha huyo.

WASHIRIKI...



Washiriki wa mbio za kilomita 21 (Tigo Half Marathon), wakikimbia wakati wa mashindano ya Kilimanjaro Marathon yaliofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Maofisa michezo kufikisha elimu mikoani*

Na Joseph Mchekadona

MAOFISA michezo na walimu wa elimu maalum kutoka mikoa tisa hapa nchini, wameahidi kuifikisha elimu ya michezo jumuishi katika mikoa yao.

Ofisa Michezo wa Wilaya ya Songwe, Mtaka Chibwi, alisema jana jijini Dodoma kuwa, mafunzo hayo yamemjenga kwa kiasi kikubwa kwani awali hakuwa na uelewa kuhusu michezo jumuishi.

Chibwi alipongeza hatua hiyo na kuahidi kutoa elimu aliyoipata kwa wenzake.

Alisema kuwashirikisha maofisa michezo kwenye tukio hilo kutasaidia utekelezwaji wenye ufanisi katika majukumu yao.

Mratibu wa Special Olympics mkoani Songwe, Anita Zubery, alisema mafunzo waliyoyapata ni mazuri kwao kwani yamewaongezea uelewa kuhusu michezo na watoto wenye ulemavu wa akili.

Mratibu wa Special Olympics mkoani Tabora, Kelvin Mlyansi, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuimarisha jamii kuhusu masuala ya unyanyapaa kwa jamii kwa sababu ya kucheza kwa ushirikiano.

Ofisa Elimu Maalum Singida Vijijini, Pendo Salvatory, alishukuru kupata nafasi ya kushiriki mafunzo hayo kwani walihitaji sana taaluma kuhusu michezo kwa walemavu wa akili.

Salvatory alisema cheti alichopokea kutoka Special Olympics Tanzania, ni fimbo kwake na pia ndio wameanza kazi rasmi.

Ofisa Michezo Mkoa wa Mara, Evance Sangawe, yeye alisema michezo jumuishi ni jambo jipya alilojifunza na kuahidi kufikisha ujumbe kwa jamii.

Sangawe alitoa ushauri kwa Special Olympics Tanzania inapotolewa elimu kama hiyo, washiriki wawe ni kwa nchi nzima kuanzia wanapokwenda kufanya vikao na wadau ili kufanikisha mashindano ya mkoa.

Katika mafunzo hayo yaliyodhaminiwa na Mfalme wa Abu Dhabi, Mohamed Bin Zayed, na kufanyika jijini Dodoma, yalianza Februari 22 na kumalizika Februari 23, mwaka huu na yanaendelea katika mikoa mingine hapa nchini kama Singida na kwinginepo.

Mikoa iliyoshiriki mafunzo hayo ni Kagera, Morogoro, Tanga, Rukwa, Ruvuma, Tabora, Singida, Songwe na Mara.

## Zimamoto: Kazi ipo ubingwa Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu ya Zanzibar mzunguko wa lala salama imeendelea kuchanja mbuga huku timu nne za juu katika msimamo zikiendelea kuchuana vikali kwenye mbio za ubingwa wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Kinara wa ligi hiyo, JKU SC imejikuta katika wakati mgumu kwa kukubali kupoteza michezo mitatu mfululizo kati ya minne iliyocheza katika mzunguko huu.

Vinara hao wana alama 40, wakifuatiwa kwa karibu na Bingwa Mtetezi, KMKM SC, yenye alama 38, wakati nafasi ya tatu ikishikiliwa na Zimamoto yenye pointi 36 sawa na timu ya KVZ FC ambayo ipo nafasi ya nne.

Ligi hiyo mpaka sasa licha ya kubaki mizunguko 11 kufikia tamati kwa msimu huu, hakuna timu ambayo unaweza kutabiri kuwa itanyakuwa ubingwa huo kutokana na ukaribu wa alama na ushindani uliopo kwa sasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa Zimamoto FC, Mohmed Hilali 'Tedy', alisema ingawa mipango yao ipo katika mbio za ubingwa, lakini bado ligi ni ngumu.

Alisema timu zote zinaonesha upinzani mkali bila kujali nafasi iliyopo katika msimamo wa ligi kwa kuwa zinahitaji kupata alama zitakazoziweka sehemu salama.

Alisema katika mchezo wao uliopita ambao waliwafunga vinara wa ligi hiyo, JKU SC mabao 4-0, ndio pekee uliokuwa mgumu zaidi tangu kuanza kwa msimu huu.

"Ligi mpaka sasa ni mapema kutabiri nani atakuwa bingwa licha ya kubakia michezo 11, timu zote zikishuka uwanjani zina uchu wa kupata alama tatu, hivyo inasababisha mwalimu kupanga kikosi cha ushindi na kuwatoa hofu wachezaji," alisema

Hata hivyo, alisema bado ana matumaini makubwa ya kutwaa taji hilo msimu huu kutokana na michezo iliyobaki.

Mzunguko wa 20 wa ligi hiyo utaendelea Alhamisi wiki hii kwa kupigwa michezo mitatu katika Uwanja wa Finya, Pemba ambapo wenyeji Hard Rock watawakaribisha Wanajeshi wenzao wa Kipanga FC.

Kwa upande wa Unguja itapigwa michezo miwili ambapo katika Dimba la Mau A, KMKM SC watavaana na Ngome FC na Dimba la Mau B, 'Wekundu wa Mji Mkongwe, Malindi SC watawakaribisha Maendeleo FC kutoka Pemba michezo yote ikichezwa saa kumi alasiri.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VARANE ATAKIWA MADRID
REAL Madrid imeanza kutathmini upya uwezekano wa kumsajili tena beki wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30 na kiungo wa kati wa Brazil Casemiro (32), ambaye klabu hiyo ya Hispania ilimuuza kwa Manchester United. (***Fichajes***)

### MBAPPE UHAKIKA MADRID
RAIS wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas, amesema kuna "uwezekano asilimia 99" kwamba mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25, atajiunga na Real Madrid baada ya kuondoka Paris St-Germain msimu wa majira ya joto. ***(L'Equipe)***

### BRUYNE AKOMALIWA SAUDIA
KLABU ya Manchester City imeweka bei ya pauni milioni 100 kwa kiungo, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 32, baada ya kutakiwa huko Saudi Arabia. ***(Talksport)***

### GALLAGHER AWANIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur ilijadiliana na Chelsea kumhusu kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, Januari na Spurs wanapanga kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### LIVERPOOL NA MAKOCHA
LIVERPOOL imewaorodhesha wachezaji Ruben Amorim wa Sporting Lisbon mwenye umri wa miaka 39 na Mjerumani, Julian Nagelsmann (36), kama mbadala iwapo watashindwa kumpata Kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso kuchukua nafasi ya kocha anayeondoka, Jurgen Klopp. (***Telegraph***)

### DE JONG KUBAKISHWA
MKURUGENZI wa michezo wa Barcelona, Deco, amesema klabu hiyo inanuia kuwabakisha kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 26 na mlinzi wa Uruguay, Ronald Araujo (24), katika klabu hiyo licha ya wawili hao kuhusishwa na uhamisho. (***Goal***)

### HERNANDEZ ALENGWA BAYERN
MLINZI wa AC Milan na Ufaransa, Theo Hernandez mwenye umri wa miaka 26, ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na Bayern Munich kuchukua nafasi ya mchezaji wa Kimataifa wa Canada, Alphonso Davies (23), ambaye atauzwa na klabu hiyo ya Ujerumani msimu wa majira ya joto ikiwa hatasaini mkataba mpya. (***Sky Germany***)

### PHILLIPS KUREJESHWA LEEDS
LEEDS United ina nia ya kumrejesha kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, katika klabu hiyo iwapo watapandishwa daraja hadi Ligi Kuu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kwa sasa yuko kwa mkopo West Ham akitokea Manchester City. (***Football Insider***)

### SZYMANSKI ATAJWA ARSENAL
ARSENAL, Manchester United na Tottenham Hotspur, zinatazamiwa kuwania saini ya kiungo wa kati wa Fenerbahce, Sebastian Szymanski, kuelekea msimu wa majira ya joto, huku AC Milan na Inter Milan pia zikimwania mchezaji huyo wa Kimataifa wa Poland mwenye umri wa miaka 24. ***(Teamtalk)***

### GREENWOOD KUBAKI GETAFE
MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22, anataka kubakia Getafe, kwa mujibu wa rais wa klabu hiyo, Angel Torres. Mshambuliaji huyo kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu hiyo ya Hispania. (***Metro***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL TUNAISHI KWENYE NDOTO ZETU - ODEGAARD

**LONDON,** England

USHINDI wa sita mfululizo kwenye Ligi Kuu England, mabao 25 yakufunga na kufungwa matatu pekee - Arsenal wapo kwenye mpambano wa kuwania taji na wanaonekana kudhamiria kubakia hapo.

**'Washikabunduki' hao bila shaka, walikuwa katika hali kama hiyo mwaka jana kabla ya changamoto yao kuporomoka, lakini wanaonesha njaa na ustahimilivu unaoashiria kuwa wamedhamiria kutorudia makosa ya hapo awali.**

"Tunaishi katika ndoto," alisema nahodha wa Arsenal, Martin Odegaard, akiiambia TNT Sports baada ya timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Newcastle United juzi na kubakisha pengo la pointi mbili nyuma ya vinara, Liverpool.

**●●● Msimu uliopita tulikosa taji na sasa ni wakati wa kuonesha kwamba tumejifunza, kila...**

"Sote tuna ndoto ya kuwa hapa. Unaona kila wiki jinsi ushindani ulivyo na hapo ndipo tunapotaka kuwa - tunataka kupigania mataji."

Wakati Arsenal wameshinda kila mechi ambayo wamecheza kwenye Ligi Kuu mwaka 2024, walipoteza mbele ya Porto katika mechi ya mkondo wa kwanza wa hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katikati ya wiki, wakiruhusu bao la dakika za lala salama.

Lakini walijibu kwa mtindo na mabao manne katika ushindi wa 4-1 dhidi ya Newcastle Jumamosi.

"Wanaonekana kama timu iliyokasirishwa sana na uchezaji wa katikati ya wiki. Vyombo vyao vya habari na ukali wao ulikuwa mzuri - mara moja kwenye mguu wa mbele," alisema mlinzi wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand.

"La msingi ni kuhakikisha hawaruhusu hofu kuingia ndani, hiyo itakuwa rahisi. Lakini hakuna dalili ya hilo kwa sasa.

"Wamekuwa timu na kitengo chenye ufanisi sana hivi sasa."

Odegaard aliongeza: "Mwaka mmoja kabla tulikosa Ligi ya Mabingwa Ulaya na tukarejea na nguvu zaidi.

"Msimu uliopita tulikosa taji na sasa ni wakati wa kuonesha kwamba tumejifunza - kila tunapocheza tunafurahi sana."

# MAN UNITED IPO KWENYE MWELEKEO SAHIHI - TEN HAG



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amesema klabu hiyo inaelekea katika "mwelekeo sahihi" licha ya kufungwa na Fulham na kuongeza kuwa "picha kubwa inaonekana nzuri sana" katika klabu hiyo.

Fulham ilishinda mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Old Trafford Jumamosi katika mchezo wa kwanza wa United tangu kuthibitishwa rasmi kwa Sir Jim Ratcliffe kununua hisa katika klabu hiyo.

Matokeo hayo yameiacha timu ya Ten Hag pointi nane kutoka kwenye nafasi nne za juu zikiwa zimebakia mechi 12, lakini kocha huyo wa Uholanzi alisema anatumaini Ratcliffe anaangalia zaidi ya kile kinachogeuka kuwa kampeni mbaya.

"Baada ya kushindwa mara moja lazima uone picha kubwa, na picha kubwa inaonekana nzuri sana," alisema Ten Hag.

"Tunatakiwa kukaba katika nafasi fulani na kuwarejesha majeruhi, kisha tutakuwa na usawa zaidi na pia kuimarisha kikosi kwenye dirisha la usajili.

"Unaona kuna wachezaji wengi wazuri wanaokuja na wenye uwezo wa hali ya juu. Watakuwa bora zaidi, kwa hiyo bila shaka tunaenda katika mwelekeo sahihi," alisema.

Fulham ilihitaji bao la ushindi dakika ya 97 kutoka kwa Alex Iwobi ili kupata ushindi wao wa kwanza Old Trafford tangu 2003 baada ya bao la kusawazisha la Harry Maguire dakika ya 89 akisawazisha lile la Calvin Bassey la katikati ya kipindi cha pili.

Baadaye, Ten Hag alizungumzia orodha yake ya majeruhi ambayo sasa inawajumuisha Luke Shaw na Rasmus Højlund. Casemiro alianza mchezo huo lakini alilazimika kutolewa nje kipindi cha pili kwa sababu ya jeraha la kichwa.

"Kwa hiyo tunapokuwa na wachezaji wanaopatikana, tunakuwa na timu nzuri sana," alisema Ten Hag.

"Leo tungeweza kushinda mchezo huu, hata sisi tungeshinda mchezo huu kwani timu ilionyesha kiwango kizuri. Tulikuwa na mwanzo wa polepole katika vipindi vyote viwili, bila shaka."

# Bayern yakubali yaishe kwa Davies




**MUNICH,** Ujerumani

BEYERN Munich inaamini Alphonso Davies ana uwezekano mkubwa wa kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto kuliko kusaini mkataba mpya hapo Allianz Arena, kwa mujibu wa ripoti.

Mkataba wa Davies hapo Bavaria utaendelea hadi mwaka 2025 na mazungumzo hayajaendelea juu ya makubaliano mapya, na hivyo kuongeza uwezekano wa kuondoka wakati wa majira ya joto.

Real Madrid wamekuwa wakijaribu kumshawishi Davies msimu mzima na inasemekana wanamwona kama mmoja wa walengwa wao wa uhamisho pamoja na Kylian Mbappe wa PSG.

Sky Sports Ujerumani imeripoti kuwa Madrid haitakuwa na tatizo kukubaliana na Davies na wanatarajiwa kuwapa Bayern ada ya juu zaidi ya euro milioni 50.

Lakini 'Los Blancos' wanaweza kujaribu kupunguza idadi hiyo ikiwa mkwamo wa mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada utaendelea hadi msimu wa majira ya joto.

Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern, Christoph Freund, hivi karibuni alikutana na wakala wa Davies mjini Munich, na hisia kutoka kwa mabingwa hao wa Ujerumani ni kwamba beki huyo wa kushoto ana uwezekano mkubwa wa kuuzwa katika dirisha la majira ya joto.

Beki ya kushoto imekuwa na tatizo pale Madrid hadi sasa msimu huu, huku Ferland Mendy akizunguka ndani na nje ya timu kutokana na jeraha na usajili wa majira ya joto wa Fran Garcia ambaye ameshindwa kutumia vema mechi zake chache hadi sasa.

Kiungo Eduardo Camavinga amelazimika kujaza nafasi ya beki wa kushoto katika mechi mbalimbali kwa mwaka mzima.



# Xavi: Sijutii kuondoka Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, amesema hajutii uamuzi wake wa kujiuzulu mwishoni mwa msimu huu baada ya ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Getafe Jumamosi kwenye Uwanja wa Olympic.

Raphinha, Joao Felix, Frenkie de Jong na Fermin Lopez kila mmoja alifunga bao moja wakati Barca wakipanda hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, pointi tano nyuma ya viongozi Real Madrid, ambao jana Jumapili walikuwa wanacheza na Sevilla.

Barca sasa wamevuna pointi 13 kutoka pointi 15 zinazowezekana kwenye ligi tangu Xavi atangaze kwamba ataondoka majira ya joto, huku mashabiki wakiimba jina lake katika kipindi chote cha pili cha ushindi wa Getafe.

Alipoulizwa katika mkutano na waandishi wa habari kama anajutia uamuzi wake kutokana na matokeo ya timu tangu wakati huo, Xavi alisema: "Hapana.

"Nadhani ni wito sahihi kabisa. Timu imesonga mbele tangu nilipofanya hivyo na wachezaji wameonesha kiwango walichonacho (dhidi ya Getafe) na katika michezo iliyopita.

"Ninashukuru sana mashabiki wanaimba jina langu, lakini nina hakika uamuzi wangu ni sahihi kwa klabu. Mashabiki wamekuwa upande wangu na kutoka moyoni ninawathamini sana."

Barca walianza kupata shangwe baada ya bao la kwanza la Raphinha katika kipindi cha kwanza.

Felix aliongeza la pili baada ya mapumziko, akirudisha krosi kutoka kwa Andreas Christensen, ambaye alicheza tena katikati ya uwanja, huku De Jong na Lopez wakikamilisha bao.

Wakati Girona na Madrid zikiwa bado hazijacheza, Barca walimaliza siku wakiwa nafasi ya pili kwenye LaLiga, huku Xavi akisema uchezaji kama huo unahitajika kusaidia kuweka shinikizo kwa timu zingine kileleni mwa jedwali.

"Hatutatupa taulo," alisema bosi huyo wa Barca.

"Tunajua tunahitaji kushinda kila wikendi. Tumepiga hatua mbele. Kuna nafasi kubwa ya kupigania ubingwa."

# KIPA LIGI KUU AWEKA REKODI CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa zamani wa Azam FC, David Kissu, ameweka rekodi ya kuwa kipa wa kwanza kufunga bao kwenye Ligi ya Championship msimu huu.

Hata hivyo, hakuna rekodi inayoonyesha kuwa kuna kipa aliwahi kufunga bao kwenye ligi hiyo tangu mfumo huo ulipoanzishwa kutoka kuwa Ligi Daraja la Kwanza, misimu miwili iliyopita.

Kissu ambaye ameshawahi kuichezea Gor Mahia ya Kenya na sasa akiidakia Biashara United inayocheza Ligi ya Championship, alifunga bao hilo dakika ya tano katika mechi iliyochezwa mwishoni mwa wiki dhidi ya Polisi Tanzania.

Alipiga 'golikiki' iliyokwenda moja kwa moja wavuni, huku kipa wa Polisi Tanzania akiwa amesogea kwenye lango lake, mpira ukampita juu na kujaa wavuni, likiwa ni bao la kwanza katika mechi hiyo iliyoisha kwa timu yake kushinda mabao 2-0.

Ushindi huo umeipeleka Biashara United hadi kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo kutafuta timu zitakazopanda Ligi Kuu msimu ujao.

Mpaka sasa Biashara United, iliyoshuka daraja msimu wa 2021/22, ipo nafasi ya pili, ikiwa na pointi 49, ikicheza mechi 22, kushinda michezo 15, sare nne na kupoteza mitatu.

Wakati Kissu akiweka rekodi hiyo, golikipa wa timu ya Ken-Gold, Castor Mhagama, yeye anaongoza kwa kukaa mechi nyingi bila kuruhusu wavu wake kutikiswa 'clean sheets.'

Kipa huyo amekaa langoni mechi 14 bila kuruhusu wavu wake kutikiswa hivyo kuongoza kwa 'clean sheets' katika ligi hiyo.

Kissu ana 'clean sheets' tisa, wakati kipa wa zamani wa Simba ambaye kwa sasa anaichezea Mbeya City, Jeremiah Kisubi, akiwa na 'clean sheets' nane.

Mhagana anaifanya timu yake ya KenGold kuongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 50 mpaka sasa.




Waziri wa Michezo na Utamaduni, Dk. Damas Ndumbalo (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni tatu mshindi wa kwanza wa mbio za kilomita 21 (Tigo Half Marathon), kwa upande wa wanawake, Faulina Matanga, katika mashindano ya Kilimanjaro Marathon yaliyofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watanzania wafunika Kili Marathon

INATOKA UK 24

ambao ni pamoja na Tigo- Km 21 (Half Marathon), Gee Soseji – Kilomita tano (Fun Run), wadhamini wa meza za maji maeneo wanayopitia wakimbiaji, ambao ni pamoja Simba Cement, Kilimanjaro Water, TotalEnergies, Benki ya CRDB, TPC Sugar, Garda World Security, CMC Automobiles, Salinero Hotels na wauzaji - Kibo Palace Hotel na Keys Hotel," alisema.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji wa TBL ambao ndio wadhamini wakuu wa hafla hiyo tangu ilipoanzishwa mwaka 2003, Michelle Kilpin, alisema tukio hilo limepiga hatua kubwa wakati likiingia mwaka wake wa 22.

"Mafanikio haya yameshuhudiwa na mamilioni ya watu duniani kote, imekuwa ni safari ya kusisimua kwani haya ni moja ya mashindano makubwa ya kimataifa ya riadha katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki, yanawaleta pamoja zaidi ya wakimbiaji 12,000 na watazamaji wengi zaidi kutoka Tanzania na nje ya nchi ambapo mwaka huu, ilihusisha washiriki kutoka nchi 56," alibainisha.

Alisema Kilimanjaro Premium Lager imetenga jumla milioni 28/- kama zawadi kwa ujumla.

Katika mbio za Km 42, Augustino Sulle kutoka Tanzania aliibuka mshindi baada ya kutumia saa 02:21:06, mbele ya Abraham Kosgei kutoka Kenya aliyetumia saa 02:22:02 na kushika nafasi ya pili, huku Elisha Kimutai pia kutoka Kenya akitumia saa 02:22:17 na kushinda nafasi ya tatu.

Kwa upande wa wanawake, Natalia Sulle alishinda baada ya kutumia saa 02:51:23 na kushinda mbio hizo, huku akimtangulia Mtanzania mwenzake Neema Sanka aliyetumia saa 02:51:47 wakati Vailet Kidasi akishinda nafasi ya tatu baada ya kukimbia kwa saa 03:01:03 na hivyo kukamilisha ushindi wa Watanzania kwa nafasi zote tatu za kwanza katika kitengo cha kilomita 42.

Katika mbio za Tigo Half Marathon Km 21, kwa upande wa wanaume ushindi ulienda kwa Faraj Damas kutoka Tanzania aliyetumia saa 01:16:40, akifuatiwa na Peter Mwangi kutoka Kenya aliyetumia saa 01:03:44, huku Mtanzania Kennedy Abel akishika nafasi ya tatu baada ya kukimbia kwa saa 01:04:22.

Kwa upande wa wanawake mbio hizo za Tigo Half Marathon, zilizotawaliwa na wanariadha wa Kitanzania, Failuna Matanga alishinda mbio hizo baada ya kutumia saa 01:16:40, Neema Kisuda akashika nafasi ya pili kwa kukimbia kwa muda wa saa 01:16:54, huku Neema Mbua pia kutoka Tanzania akishika nafasi ya tatu baada ya kukimbia kwa saa 01:17:07.

Katika mbio hizo za kilomita 21, Tigo Half Marathon, Vivian Opskvik kutoka Norway alishika nafasi ya tisa baada ya kutumia saa 01:29:09, jambo ambalo lilonyesha msisitizo kuwa mbio hizo ni za kimataifa.

# TPLB yazipongeza Simba, Yanga CAF

**Na Shufaa Lyimo**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imezipongeza timu za Simba na Yanga kwa kufanya vizuri katika michezo yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo, alisema, Simba imefanya kazi kubwa kupata pointi moja muhimu ikiwa ugenini dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, wakati Yanga ikifanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali baada ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria kwenye iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi.

"Ninazipongeza Simba na Yanga kwa kufanya vizuri katika michezo yao ya kimataifa. Yanga imeonyesha uwezo mkubwa na kuweza kuingia hatua ya robo fainali kwa kuifunga timu ya CR Belouizdad kwa idadi kubwa ya mabao, lakini Simba pia ilipata pointi moja muhimu ugenini, naamini mchezo wa nyumbani itafanikiwa na kusonga mbele," alisema Kasongo.

Mtendaji huyo wa TPLB, alisema kutokana na ubora wa timu ya Simba, anaamini itapata matokeo mazuri itakapoikaribisha Jwaneng Galaxy, kwani Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, anafanya juhudi kubwa kuhakikisha michezo inazidi kukua.

"Ni wakati wa Watanzania kuungana pamoja na kujitokeza kwa wingi ifikapo tarehe mbili (mwezi ujao) kwa ajili ya kuisapoti timu yetu, kufanikiwa kwa Simba ni furaha ya Taifa kwa ujumla," alisema Mtendaji huyo.

Aidha, aliongeza kuwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kushirikiana na TPLB wamepanga mikakati ya muda mrefu kuhakikisha timu zetu zinafanya vizuri nje na ndani ya nchi.

"Ni mipango yetu ya muda mrefu ambayo tumejiwekea kuhakikisha timu zetu zinafanya vema kwenye mashindano ya Kimataifa nje na ndani ya nchi, mafanikio tumeanza kuyaona," alisema.

# *Gamondi apania ...*

INATOKA UK 24

Abdelhak Benchikha, amesema kazi iliyobaki ni kufanya marekebisho madogo kwenye safu ya ushambuliaji kwa ajili ya kumalizia kazi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jumamosi dhidi ya Jwaneng Galaxy.

Wakati kocha huyo akisema hayo, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, ametamba kwao kuingia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa ni jambo lisilo na shaka kwani wameshafanya hivyo mara nne, na wamekuwa wakifanya hivyo katika mechi nyingi za maamuzi zinazochezwa Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ahmed amewatoa shaka wanachama na mashabiki wa Simba kuwa hakitatokea kile kilichotokea Oktoba 24, 2021 ilipofungwa mabao 3-1, Uwanja wa Banjamin Mkapa na timu hiyo kiasi cha kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa kabla ya kuangukia Kombe la Shirikisho ambako ilikwenda hadi hatua ya robo fainali.

Alisema uzuri ni kwamba wanajua kwa nini walifungwa na jambo hilo kamwe halitajitokeza tena, kwa sababu walishafanikiwa kulidhibiti.

"Tunatarajia kutua nyumbani alfajiri ya Jumatatu, tukifika mara moja tunaanza maandalizi ya dhidi ya Jwaneng Galaxy, Machi 2, hatuna mchezo wowote wa ligi hapo katikati, ila tunasubiri taarifa kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), kuhusu mchezo wetu wa kiporo wa Kombe la FA dhidi ya TRA, kama utakuwapo tutacheza," alisema Ahmed.

# Michezo

Nipashe

Jumatatu Februari 26, 2024




Arsenal tunaishi ndoto zetu - Odegaard UK. 21

# Watanzania wafunika Kili Marathon




Waziri wa Michezo na Utamaduni, Dk. Damas Ndumbalo (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni tano mshindi wa kwanza wa mbio za kilomita 42, Augostino Sulle, katika mashindano ya Kilimanjaro Marathon yaliofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro jana, wa pili kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Michelle Kilpin. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Jumanne Juma,** MOSHI

MBIO za Kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager Marathon zimeendelea kuwa kivutio cha watu wengi kiasi cha kufanya shughuli mbalimbali kusimama katika mji wa Moshi, Kilimanjaro wakati tukio la 22 la mashindano hayo yaliyofanyika jana mkoani humo huku washiriki kutoka Tanzania wakiendelea kufanya vizuri.

Idadi kubwa ya watu kutoka ndani na nje ya nchi walishiriki katika mbio hizo ambazo zilishirikisha zaidi ya wakimbiaji 10,000, mbio hizo zikijumuisha Kilimanjaro Premium Lager Km 42, Tigo Half Marathon Km 21 na Gee Soseji Fun Run kilometa tano.

Waziri wa Michezo, Utamaduni na Michezo, Damas Ndumbaro, ndiye aliyeanzisha mbio hizo, ambapo pia alishiriki na kumaliza mbio za kilomita tano za kujifurahisha na baadaye alikuwa kwenye mstari wa kumaliza kupokea washiriki waliomaliza mbio hizo wakiwamo washindi wa vipengele vyote.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Waziri Ndumbaro aliwapongeza waandaaji wa mbio hizo ambazo alisema zimechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha michezo nchini pamoja na kuibua vipaji vipya kila mwaka.

"Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na waanzilishi wa mbio hizi, pamoja na wadhamini wakuu na wadau wengine wa michezo katika kuhakikisha mbio hizi zilizoanzishwa zaidi ya miaka 20 iliyopita zinakuwa endelevu kwa manufaa ya maendeleo ya michezo nchini.

"Nichukue fursa hii kuwashukuru wadhamini wakuu wa mashindano ya Kilimanjaro Premium Lager na wadhamini wengine

INAENDELEA UK 23

# GAMONDI APANIA KUIDUWAZA AL AHLY

## ●●● Rais Samia aipongeza Yanga, Benchikha naye asema robo fainali Simba lazima, lakini...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuiongoza Yanga kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku akiwa na mechi moja mkononi, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amewapongeza wachezaji wake kwa ushindi mkubwa wa mabao 4-0 dhidi ya CR Belouizdad juzi, huku akisema sasa wanataka pointi katika mchezo wa mwisho, Ijumaa wiki hii dhidi ya Al Ahly nchini Misri.

Akizungumzia kuhusu mechi hiyo ya juzi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Gamondi alisema walianza vibaya mechi za hatua ya makundi na watu waliwachukia na kutokuwa na furaha, lakini jana wamekuwa bora na yeye amewasamehe waliokuwa hawana furaha kwani ndio mpira ulivyo, sasa wanaangalia mbele.

Alisema kwenye mpira ukitengeneza nafasi unatakiwa kuzitumia, lakini si zote unaweza kuzitumia ila walichokifanya wachezaji wake juzi ni kizuri.

"Tumeshafuzu bila kujali matokeo ya mechi iliyobaki, lakini tunaenda kutafuta pointi ugenini dhidi ya Al Ahly, ninaifahamu vizuri, tutaenda kucheza kwa kufurahi bila ya presha.

"Kwa kuwa tunahitaji alama katika mchezo huo ili tumalize kwa heshima tunaenda kufanyia kazi ubora wao na kusahihisha makosa yetu kwa ajili ya kutafuta heshima katika mchezo wetu wa mwisho," alisema Gamondi.

Kocha wa CR Belouizdad, Mbrazili Marcos Paquette, alisema mashindano ni magumu kwao na kwamba walicheza na timu bora, hivyo walijaribu kucheza vizuri lakini wamekutana na ugumu.

Aliongeza kuwa pia joto lilikuwa kali kwa wachezaji wake walichoka haraka na kushindwa kufanya vizuri katika dakika za mwanzo za kipindi cha pili na kuruhusu mabao mawili ya haraka haraka baada ya mapumziko.

"Matokeo ya Yanga kwa sasa yametukatisha tamaa, lakini hatutachoka tunaenda kupambana kujiandaa na mechi ya mwisho dhidi ya Medeama FC, tutatumia mchezo huu kuangalia makosa na kusahihisha kabla ya mechi yetu ya mwisho," alisema Marcos.

Katika hatua nyingine, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suhuhu Hassan, ameipongeza Klabu ya Yanga kwa kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kupitia akaunti yake ya Instagram jana, Rais Samia, alisema ushindi wa Yanga umeandika historia kubwa kwa klabu hiyo na sekta ya michezo nchini, lakini umeleta furaha kwa mamilioni ya mashabiki wa timu hiyo na Watanzania kwa ujumla.

"Naipongeza Klabu ya Yanga kwa kufanya vyema katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), na kufanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali.

"Mafanikio haya yameandika historia kubwa kwa klabu na sekta ya michezo nchini. Mmeleta furaha kwa mamilioni ya mashabiki wenu na Watanzania kwa ujumla," aliandika Rais Samia.

Kwingineko kwa upande wa Simba ambayo Ijumaa ilitoka suluhu ugenini dhidi ya Asec Mimosas, Kocha Mkuu,

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >